**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**OFISI YA RAIS-FEDHA NA MIPANGO**

# HOTUBA YA BAJETI YA SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR KWA MWAKA FEDHA 2025/2026

**DKT. SAADA MKUYA SALUM (MBM)**

**WAZIRI WA NCHI-OFISI YA RAIS,**
**FEDHA NA MIPANGO**

**JUNI, 2025**



**Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi**
**Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi**

***"Tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie Kuendelea kuwa wamoja na Kushirikiana kwa Manufaa ya Nchi yetu. Tuvuke Kipindi hiki kwa Salama ili kizazi cha sasa na Kijacho Kifurahie Ustawi wa Taifa Letu"***

Baraza la Eid El Fitri, 31 Machi, 2025.

YALIYOMO

A. UTANGULIZI ........................................................1
B. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2024/2025 ........................................4
B.1 Mapato ........................................................4
B.2 Matumizi ........................................................6
C. DENI LA TAIFA ........................................................7
C.1 Uhimilivu wa Deni la Taifa ........................................................8
D. MISAMAHA YA KODI ........................................................8
E. UTEKELEZAJI MAPENDEKEZO YA SERA ZA KUIMARISHA MAPATO KWA KIPINDI CHA JULAI 2024-MACHI 2025 ........................................10
E.1 Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Namba 4 ya Mwaka 1998 ........................................10
E.2 Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Namba 8 ya Mwaka 2017 ........................................11
E.3 Marekebisho ya Sheria ya Fedha Namba 9 ya Mwaka 2015 12
E.4 Marekebisho ya Sheria ya Ada ya Huduma za Bandari namba 2 ya Mwaka 1999 ........................................13
E.5 Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Namba 7 ya Mwaka 2013 ..................14
F. MAFANIKIO YA SERIKALI KWA KIPINDI CHA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 ........................................17
G. MAFANIKIO YA SERIKALI KWA KIPINDI CHA MUHULA WA KWANZA WA AWAMU YA NANE ........................................22
H. MATARAJIO YA MAPATO NA MATUMIZI JULAI-JUNI KWA MWAKA 2024/2025 ........................................55
I. MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2025 .57
J. MAPENDEKEZO YA HATUA ZA KUIMARISHA UCHUMI NA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 .............58
K. MAPENDEKEZO YA SURA YA BAJETI MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ........................................67
L. VIPAUMBELE VYA KIBAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ........................................69

M. UGHARAMIAJI WA NAKISI YA BAJETI ........................... 75
N. HALI YA UTEGEMEZI KWA MWAKA 2024/2025 ............ 75
O. MAZINGATIO YA MAENEO MAHSUSI KWA BAJETI YA 2025/2026 ............................................................ 76
P. SHUKURANI ............................................................ 79
R. HITIMISHO ............................................................. 84

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Sina budi kuanza na shukurani zangu kwa Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataala, kwa kuendelea kuturuzuku neema yake ya pumzi, siha na kutubarikia kila neema amani na upendo inayoendelea kutawala ndani ya visiwa vya Unguja na Pemba Alhamdulillah. Kila Mwanaadamu anapaswa kushukuru kwa kadiri Allah anavyotupangia kwa mujibu wa imani zetu, huku tukiamini **'Kheri zinatokana na Muumba!**

2. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Katiba ya Mwaka 1984 na Sheria ya Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016 zote kwa pamoja, zinamuwajibikia Waziri mwenye dhamana ya Fedha kutayarisha na kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali, kwa mwaka unaofuata wa fedha mbele ya Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kujadiliwa na kuidhinishwa.

3. **Mheshimiwa Spika,** Nakushukuru sana kwa fursa niliyoipata nikiwa kama Waziri wa Nchi-Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa kipindi cha miaka mitatu na nusu sasa, kuweza kutimiza wajibu huo ulio chini ya Kifungu cha 105 cha Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 (kama ilivyorekebishwa) na Kifungu cha 41(3) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2016.

4. **Mheshimiwa Spika,** Kabla ya kuendelea mbele naomba kutoa hoja ya kuwa Baraza lako lipokee, lijadili na kukubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

5. **Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati kabisa naomba nitoe shukurani za kipekee, kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Makamu wake Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango,

Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa na Naibu Waziri Mkuu Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko. Kiukweli nahisi nastahiki kutoa neno zaidi ya shukurani, ila kwa mila na maadili yetu ya kitanzania neno shukurani linathamani zaidi. Tunathamini mno uongozi wao imara, dhamira yao ya kweli ya kuleta maendeleo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na ushirikiano mzuri wanaouendeleza kwa Zanzibar na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hii imepelekea muunganiko wa hali ya juu kwa pande zote katika shughuli za kiuchumi, kijamii na kiutawala.

6. **Mheshimiwa Spika,** Tumeshuhudia shughuli mbalimbali za kitaifa kufanyika pande zote mbili za Muungano ikiwemo viapo kwa viongozi wa Serikali, vikao vya Baraza la Mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, utoaji wa tunzo kwa viongozi wakuu na matamasha mbalimbali likiwemo Tamasha la Kizimkazi lililoteka hisia za watanzania wengi wakiwemo wasanii wakubwa nchini pamoja na watalii. Hii imeweka wazi si kuwa tumeungana kwa kuchanganya mchanga na muingiliano wa damu tu bali ina maana kubwa zaidi kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

7. **Mheshimiwa Spika,** Natumia fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Uendeshaji wa uongozi wake umekuwa wa umahiri mkubwa, hekima, uvumilivu wa kupigiwa mfano na uadilifu wa hali ya juu, uliopelekea kuimarisha umoja, amani na maendeleo ya kiuchumi na kijamii ambayo kwa ufupi tutayagusia ndani ya Hotuba yangu hii.

8. **Mheshimiwa Spika,** Dkt. Hussein Ali Mwinyi anaendelea kutimiza maono na matamanio yake ya kuifanya Zanzibar kuwa kama miji mengine mikubwa inayotambulika kimataifa. Kwa hakika yale yaliyodhaniwa kuwa magumu

sasa yamewezekana, na yaliyokua yanaonekana kuwa hayawezekani yamegeuka kuwa halisi na yale ambayo tulikuwa tunafikiria kuwa ni ndoto za Alinacha zimekuwa ndoto za kweli. Kinachoonekana ndio hali halisi ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 pamoja na ahadi zake wakati wa mikutano ya kampeni.

9. **Mheshimiwa Spika,** Wengi wetu wakati tuko wadogo tulikuwa tunaamini na kudhani kuwa siasa maana yake **ni ahadi zisizokuwa za ukweli,** na hata mazungumzo yetu huthubutu kusema anazungumza **siasa** tu! **Tukimaanisha hakuna utekelezaji wa anachokizungumza.** Nathubutu kusema kwa sasa Wazanzibari tumepata somo juu ya maana halisi ya siasa kupitia Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi **Dkt. Hussein Ali Mwinyi.** Ameondoa dhana na maana ambayo ilituwama ndani ya mioyo na akili zetu. Tumeshuhudia utekelezaji wa ahadi nyingi zilizotolewa katika mikutano mbalimbali ya kampeni, zikiwemo; ujenzi wa masoko, uwezeshaji wa mitaji kwa wajasiriamali, vitambulisho kwa wafanya biashara wadogo wadogo, ugawaji wa boti kwa wavuvi, barabara za lami maeneo yote, miundobinu mengine ya usafiri, ujenzi wa bandari na mingi mengineyo.

10. **Mheshimiwa Spika,** Mengi yamefanyika na kila Wizara ilijaribu kwa kiasi kikubwa kuwasilisha mafanikio ya sekta yake katika hotuba za bajeti zao wakati wa kupitisha mafungu ya bajeti. Tumeyasema na kuyaona lakini kipindi hichi '***Mkasi ndo umekuwa shuhuda, na kazi ya mkasi ya kukata utepe ilikuwa kubwa mno mpaka maneno ya kuzungumza yakawa yameisha'!***

11. **Mheshimiwa Spika,** Nikiri kuwa mafanikio makubwa yaliyopatikana kupitia awamu zote yana mchango mkubwa, kupitia wasaidizi wa karibu wa marais katika vipindi vyao vya uongozi katika maendeleo ya Zanzibar. Tumeshudia

uthubutu wa hali ya juu kwa viongozi wetu, wakitekeleza majukumu yao kwa kiwango cha ziada ili kuhakikisha uchumi wa Zanzibar unakuwa kwa **kasi ya 5G.** Kwa hili, sina budi kuwapongeza wasaidizi wa karibu wa Mheshimiwa Rais, Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa **Othman Masoud Othman** na Makamu wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah. Kwa hakika wanajitoa kulitumikia Taifa.

12. **Mheshimiwa Spika,** Kwa sasa naomba uniruhusu niendelee na kuwasilisha taarifa kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2024/2025 kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025.

## B. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2024/2025

13. **Mheshimiwa Spika,** Kabla ya kuwasilisha tathmini ya Mapato na Matumizi ya miezi tisa naomba Taarifa za Mwenendo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar nilizowasilisha asubuhi ya leo wakati wa uwasilishaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2025/2026, ziwe ni sehemu ya Hotuba yangu hii.

### B.1 Mapato

14. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali ilipanga kukusanya **TZS 5,182.89 bilioni** kutoka vyanzo vyote vya ndani na nje hadi kufikia Machi 31 kiasi cha **TZS 2,204.10 bilioni** zimekusanywa kwa mchanganuo ufuatao;

   i. Mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar ZRA yamefikia **TZS 655.53 bilioni** sawa na **asilimia 99.63** ya makadirio ya kipindi hicho,
   ii. Mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) upande wa Zanzibar yamefikia **TZS 471.04 bilioni** sawa na **asilimia 106.34** ya makadirio ya kipindi hicho,

iii. Mapato yasiyokuwa ya kodi, yamefikia TZS 136.65 bilioni sawa na **asilimia 68.19** ya makadirio ya kipindi hicho,
iv. Mapato ya kodi za wafanyakazi kutoka SMT (PAYE) walioko Zanzibar yalikusanywa kwa asilimia mia moja kama ilivyotarajiwa **TZS 15.75 bilioni,**
v. Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yamefikia **TZS 10.33 bilioni** sawa na **asilimia 54.53** ya makadirio ya kipindi hicho,
vi. Mapato ya Taasisi zinazojitegemea za Serikali yalifikia **TZS 129.54** bilioni sawa na **asilimia 85.82** ya makadirio ya kipindi hicho,
vii. Mikopo ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni **TZS 418.47 bilioni** sawa na **asilimia 118** ya makadirio ya kipindi hicho, na
viii. Mapato yatokanayo na misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo yamefikia **TZS 353.29** bilioni sawa na **asilimia 86.4** ya makadirio.

**15. Mhesimiwa Spika,** Kwa kipindi cha tathmini mapato ya ndani yaliyokusanywa yameonesha ukuaji wa asilimia **32** ukilinganisha na kipindi kama hicho mwaka 2023/2024, ukuaji huo umetokana na;

i. Kuimarika kwa ufuatiliaji na usimamizi wa walipakodi, ikiwemo matumizi ya mifumo ya kisasa ya TEHAMA inayowezesha ufuatiliaji wa karibu wa shughuli za biashara na ulipaji kodi.
ii. Uhamasishaji wa walipakodi kuhusu wajibu wa kulipa kodi, kupitia kampeni za elimu kwa umma na ushirikiano na wadau wa sekta binafsi.
iii. Upanuzi wa wigo wa walipakodi kwa kusajili vyanzo vipya vya mapato na kuwafikia wafanyabiashara waliokuwa nje ya mfumo rasmi wa ulipaji kodi.
iv. Ukusanyaji wa madeni ya kodi kwa kutumia mbinu mbalimbali za kisheria na kiutawala.
v. Kuimarika kwa shughuli za kiuchumi hasa katika sekta

za biashara, huduma, uwekezaji na utalii, ambazo zimechangia kuongeza kiwango cha mapato.

vi. Uwekezaji mkubwa wa Serikali katika ujenzi wa miundombinu unaotumia vifaa mbalimbali vinavyotozwa kodi, na kuongezeka kwa huduma za kijamii kumechangia kwa kiasi kikubwa kuongeza mapato ya ndani.

16. **Mheshimiwa Spika,** Upatikanaji wa fedha kutoka soko la ndani umeimarika kutokana na Serikali kutoa Hati Fungani Yenye Kufuata Misingi ya Sharia (SUKUK) sambamba na kutoa elimu kwa umma. Lengo ni kuhamasisha ushiriki katika kuwekeza kwenye Hati Fungani yenye dhamana ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Serikali imefanikiwa kupata zaidi ya asilimia 128 ya lengo iliyojiwekea kwa awamu ya kwanza.

**B.2 Matumizi**

17. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, Serikali imetumia TZS 2,383.16 bilioni sawa na asilimia 97.3 ya makadirio ya kipindi cha tathmini. Matumizi haya yanajumuisha; Matumizi ya Serikali Kuu ya TZS 2,255.10 bilioni; Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa TZS 11.42 bilioni na Matumizi ya Taasisi zinazojitegemea TZS 116.65 bilioni.

18. **Mheshimiwa Spika,** Kiasi cha TZS 1,208.47 bilioni zimetumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida, sawa na asilimia 90.84 ya makadirio. Matumizi hayo yameelekezwa katika maeneo yafuatayo;

i. Mishahara kwa wafanyakazi wa Serikali na Taasisi zinazopokea ruzuku ni **TZS 583.33** bilioni,

ii. Matumizi mengineyo ya Mafungu na Taasisi za ruzuku ni **TZS 214.05 bilioni,**

iii. Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi Zinazojitegemea ni **TZS 126.49 bilioni** na

iv. Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Huduma za Serikali ni **TZS 284.6 bilioni.**

19. **Mheshimiwa Spika,** Fedha zilizotumika kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na kuweka akiba katika Mfuko wa kugharamia Madeni ni TZS 1,174.69 bilioni sawa na asilimia 104.9 ya makadirio. Matumizi hayo ni;-
   i. Fedha za ndani **TZS 858.40 bilioni,**
   ii. Misaada na Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, **TZS 151.93 bilioni,**
   iii. Fedha zilizotumika kutekeleza Miradi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa **TZS 1.58 bilioni** na
   iv. **TZS 162.78 bilioni** zimewekwa katika Mfuko wa Kugharamia ulipaji wa Madeni yaliyokopwa kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. **Kiambatisho Nambari :1 kinahusika**

## C. DENI LA TAIFA

20. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2025, deni linalodhaminiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar limefikia **TZS 1,334.6 bilioni**. Kati ya deni hilo, deni la ndani ni **TZS 1,319.4 bilioni** sawa na asilimia 99 ya deni lote na deni la nje ni **TZS 15.20 bilioni** sawa na asilimia **1**. Deni hilo limeongezeka kwa **TZS 400.6 bilioni** ukilinganisha na deni lililo ripotiwa la Mwezi Machi 2024, lililokuwa la **TZS 934 bilioni.**

21. **Mheshimiwa Spika,** Kati ya deni la ndani la **TZS 1,319.4 bilioni**, **TZS 557.5 bilioni** linatokana na Hati Fungani za muda mrefu kutoka Benki Kuu (BoT) na **TZS 761.9 bilioni** linatokana na mikopo ya Taasisi za kifedha ikiwemo benki za (PBZ, CRDB, NBC, STANBIC) na ZSSF. Deni hili limeongezeka kwa **TZS 400.1 bilioni** sawa na asilimia **43.5** ya ongezeko ukilinganisha na deni lililoripotiwa kipindi kama hichi Mwaka 2024 la **TZS 919.3 bilioni**.

### C.1 Uhimilivu wa Deni la Taifa

**22.** **Mheshimiwa Spika,** Deni la Taifa lililoripotiwa mwishoni mwa Mwezi Machi 2025 limeonekana kuwa ni himilivu kwa kuzingatia uwiano ufuatao:

i. Thamani halisi ya deni kwa sasa ni **TZS 1,319.4 bilioni** ambapo uwiano wa deni na Pato Halisi la Taifa (GDP at Constant Price) ni **TZS 4,026.4 bilioni** limefikia kiwango cha asilimia 33.

ii. Kwa kutumia (GDP at Current Price) ya **TZS 6,572.6 bilioni** uwiano wa Deni la Taifa kwa Uchumi kwa thamani halisi limefikia kiwango cha asilimia **20,** ambapo uwiano unaokubalika kwa nchi zenye uchumi wa kati wa chini (Lower Middle Income Economies) inatakiwa kwa uwiano wa Deni la Taifa kwa uchumi usizidi asilimia **55**.

iii. Ukuaji endelevu wa mapato ya ndani kwa zaidi ya asilimia 100.

**23.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa deni lililokopwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kutekeleza miradi ya SMZ limefikia **TZS 3,067.5** bilioni na **hii ni moja ya neema na faida za Muungano wetu.**

**24.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kutafuta njia mbadala za kifedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo inachochea hali ya kiuchumi na ya kijamii kwa kuzingatia uhimilivu wa deni. Aidha, Serikali inaendelea kulipa na kulihudumia deni la Taifa pasi na kuacha mzigo wa deni lililoiva.

## D. MISAMAHA YA KODI

**25.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi, 2025 jumla ya maombi 294 ya misamaha ya kodi

kutoka Taasisi za umma na binafsi yalipokelewa. Kati ya maombi hayo, maombi 260 yamekubaliwa kutokana na kukidhi masharti ya Sheria, na maombi 34 yamekataliwa kutokana na kutokidhi masharti ya Sheria.

**26.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi hicho, misamaha iliyotolewa ilikuwa na thamani ya **TZS 119.086 bilioni,** ambapo Mamlaka ya Mapato Tanzania-TRA kwa upande wa Zanzibar imetoa misamaha ya **TZS 83.239 bilioni** na Mamlaka ya Mapato Zanzibar-ZRA imesamehe **TZS 35.847 bilioni**. Kumekuwa na ongezeko la misamaha ya kodi ukilinganisha na misamaha ya **TZS 66.41 bilioni** iliyotolewa katika kipindi kama hichi 2023/2024. Misamaha hiyo inatokana na Serikali kuendelea kutekeleza miradi ya maendeleo ya umma pamoja na miradi mbali mbali ya uwekezaji, na Taasisi zisizo za Serikali.

**27.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 miradi inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo imenufaika kwa asilimia **40** ya thamani ya misamaha yote iliyotolewa katika kipindi cha tathmini, asilimia **26** kwa Taasisi za Serikali na asilimia **34** kwa Miradi ya Uwekezaji na Taasisi zisizo za Serikali. Miongoni mwa miradi iliyopatiwa Misamaha ni pamoja na;

i. Mradi wa Ukarabati na Usafi katika Usambazaji wa Huduma za Maji,
ii. Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Maji,
iii. Ukarabati wa Jengo la Beit El Ajaib,
iv. Ukuzaji wa uchumi jumuishi Zanzibar (BIG-Z),
v. Mradi wa Kumaliza Malaria Zanzibar,
vi. Ujenzi na Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo na
vii. Ujenzi wa barabara za vijijini na barabara za ndani.

**28.** **Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, Serikali imekusudia kupitia upya masharti ya utowaji wa misamaha hii, ili misamaha itakayotolewa iwe yenye tija za kiuchumi na kijamii.

## E. UTEKELEZAJI MAPENDEKEZO YA SERA ZA KUIMARISHA MAPATO NA UCHUMI KWA KIPINDI CHA JULAI 2024 - MACHI 2025

**29. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali imeendelea kuchukua hatua kadhaa ili kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato na kuimarisha uchumi. Hatua hizo zilihusu marekebisho ya Sheria na Sera mbalimbali. Kwa kipindi cha Julai 2024, hadi Machi 2025, miongoni mwa maeneo yaliyoleta tija na kuimarisha uchumi kutokana na utekelezaji wa Sera na Sheria hizo ni pamoja na;-

### E.1 Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Namba 4 ya Mwaka 1998

#### i. Kuoanisha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) katika Huduma za Elektroniki (Digital Services)

**30. Mheshimiwa Spika,** Kufuatia mabadiliko ya Sheria ya Kodi ya ongezeko la Thamani (VAT), ZRA kwa kushirikiana na kampuni ya UBX iliweza kukamilisha uundaji wa Moduli mpya katika mfumo wa ZIDRAS mwishoni mwa mwezi wa Disemba 2024; Moduli hiyo itawezesha kuwasajili, kuwasilisha ritani na kufanya malipo kwa wafanyabiashara hao kwa urahisi. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2025 wafanyabiashara 34 na washauri wa kodi watano (5) kutoka Nje ya Nchi wameshafikiwa na kutambuliwa na kutakiwa kufanya usajili wa kulipa kodi.

#### ii. Kuoanisha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) katika Huduma za Bima

**31. Mheshimiwa Spika,** Pendekezo la kuoanisha Kodi ya Ongezeko la Thamani kuwa asilimia 18 kwa Huduma za Bima nchini ambapo utekelezaji wake umepelekea kufanyika kwa marekebisho katika mfumo wa ukusanyaji wa mapato

wa ZIDRAS katika uwasilishaji wa ritani kwa kiwango cha kodi cha asilimia 18 kwa huduma za bima nchini. Hadi mwezi Machi 2025, **TZS 3.562 bilioni** zimekusanywa ikilinganishwa na **TZS 1.958 milioni** zilizokusanywa katika kipindi kama hichi mwaka 2024 ambapo ni sawa na ongezeko la asilimia **81.9.**

### iii. Kutoa Unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Usambazaji wa Boti zinazotengenezwa Nchini

**32.** **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa lengo la kushajihisha Uwekezaji katika Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Hadi kufikia Machi 2025 Boti (fiber) 150 zenye urefu wa mita 3.5 zilitengenezwa na kupata unafuu wa kodi. Kiasi cha **TZS 40.5 milioni** zilisamehewa ili kuwawezesha wananchi kuweza kununua boti kwa bei nafuu na kuendelea na shughuli za uvuvi wakiwa na vyombo vya uhakika na vilivyo salama.

## E.2 Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Namba 8 ya Mwaka 2017

### i. Kutoa Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Uingizaji wa Gesi Nchini (Liquified Petroleum Gas - LPG).

**33.** **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho na utekelezaji wake umeanza rasmi Julai 2024 hadi kufikia Machi 2025, Gesi ya LPG yenye ujazo wa tani 4,415.53 yenye thamani ya **TZS 4.460 bilioni**, iliingizwa nchini na kupatiwa Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa wa kiasi cha **TZS 0.503 bilioni** na watumiaji 47,000 walinufaika na huduma hii na kupelekea kupungua kwa matumizi ya kuni na mkaa na ukataji wa misitu na uhifadhi wa mazingira kuimarika.

ii. Kutoza Ushuru wa Bidhaa (Excise Duty) kwa Uingizaji wa Kuku na Samaki Nchini

**34.** **Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Ushuru wa Bidhaa imefanyiwa marekebisho kwa kuweka kiwango cha TZS 300 cha Ushuru wa Bidhaa kwa kilo moja ya kuku (frozen chicken) au samaki (frozen fish) wakati wa uingizaji ili kushajiisha uwekezaji wa uzalishaji wa kuku na samaki. Hadi mwezi Machi 2025, **TZS 2.698 bilioni** zimekusanywa kwa uingizaji wa kuku na samaki nchini wa kiasi cha kilogramu 8.99 milioni. Hatua hii ilipelekea kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya samaki wanaozalishwa nchini kutoka tani 80,085 zilizouzwa kwa **TZS 569.1 bilioni** mwaka 2023/2024 na kufikia tani 78,943 zilizouzwa kwa **TZS 618.2 bilioni** mwaka 2024/2025 na hivyo kuchochea ukuaji wa kipato cha wananchi wanaojishughulisha na uvuvi nchini.

**iii. Kuongeza Kiwango cha Kutozea Ushuru wa Bidhaa kwa Uingizaji wa Mvinyo na Vinywaji Vikali**

**35.** **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kuongeza kiwango cha kutozea Ushuru wa Bidhaa kwa Uingizaji wa Mvinyo na Vinywaji Vikali. Kiasi cha **TZS 2,015.52 milioni** zilikusanywa kutokana na uingizaji wa lita 472,162 za mvinyo sawa na ongezeko la **TZS 907.51 milioni** zilizotokana na kuongezwa kwa kiwango cha Ushuru wa Bidhaa kwa uingizaji wa mvinyo na vinywaji vikali kutoka kiwango cha **TZS 2,466.45** kwa lita mpaka kiwango cha **TZS 4,386.06** kwa lita.

## E.3 Marekebisho ya Sheria ya Fedha Namba 9 ya Mwaka 2015

**i. Kutoza Kiwango Maalum cha Kodi ya Miundombinu kwa Wageni Wanaolala katika ya Visiwa au Vyumba vya Baharini**

**36.** **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa Kutoza Kiwango Maalum cha Kodi ya Miundombinu kwa Wageni wanaolala katika Visiwa au Vyumba vya Baharini.

Utekelezaji wa hatua hiyo umeanza rasmi Julai, 2024 hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha **Dola za Kimarekani 83,140** zimekusanywa ikilinganishwa na **Dola za Kimarekani 16,491** zilizokusanywa katika kipindi kama hichi mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 400.2.

**ii. Kutoza Kodi ya Miundombinu kwa Kiwango cha Dola za Kimarekani**

37. **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kuanza Kutoza Kodi ya Miundombinu kwa Kiwango cha Dola za Kimarekani kwa abiria wageni wanaonunua tiketi kwa kutumia dola za Kimarekani kwa kiwango cha Dola za Marekani 2 kwa abiria wanaosafiri kwenda Tanzania Bara na kiwango cha Dola za Kimarekani cha Dola 1 kwa wageni wanaosafiri ndani ya Zanzibar. Hadi kufikia Machi 2025, **Dola za Kimarekani 313,437.44** zimekusanywa kutokana na hatua hiyo.

**E.4 Marekebisho ya Sheria ya Ada ya Huduma za Bandari namba 2 ya Mwaka 1999**

**i. Kutoza Ada ya Huduma za Bandari kwa Kiwango cha Dola za Kimarekani**

38. **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kuanza kutoza Kodi ya Miundombinu kwa kiwango cha Dola za Kimarekani kwa abiria wageni wanaonunua tiketi kwa kutumia dola za Kimarekani kwa kiwango cha Dola 2 kwa abiria wanaosafiri kwenda Tanzania Bara na kiwango cha Dola  Dola 1 kwa wageni wanaosafiri ndani ya Zanzibar. Hadi kufikia Machi 2025, **Dola za Kimarekani 313,437.44** zimekusanywa kutokana na hatua hii.

**ii. Kuongeza Kiwango cha Ada ya Huduma za Bandari kwa Abiria Wanaosafiri Nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

39. **Mheshimiwa Spika,** Pendekezo la kuongeza kiwango cha ada ya huduma za bandari kwa abiria wanaosafiri nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaokuja Zanzibar na Meli za kitalii (Cruise Ship) au Meli ndogo za kitalii (Yacht) wanaposhuka na kutembea katika maeneo mbali mbali nchini kwa kiwango cha Dola za Marekani 15. Tangu kupitishwa marekebisho ya Sheria hii, meli nne za aina hiyo zilifika Zanzibar mwezi wa Disemba zikiwa na abiria 2,062 na kukusanya **Dola za Kimarekani 30,930**.

### E.5 Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Namba 7 ya Mwaka 2013

i. Kutoza Ada ya Udhibiti (Regulatory Levy) ya TZS 50 kwa Kilo kwa Uingizaji wa Gesi Asilia

40. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali imeanza kutoza ada ya udhibiti (Regulatory Levy) ya TZS 50 kwa kilo kwa Uingizaji wa Gesi Asilia wakati wa uingizaji bidhaa nchini. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 mapato yaliyokusanywa ni **TZS 240.30 milioni**.

## F. UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE VYA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

41. **Mheshimiwa Spika,** Wakati wa Uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2024/2025, tuliainisha hatua kadhaa za kisera katika kuimarisha uchumi na kusimamia matumizi ya Serikali yakiwemo maeneo mahsusi ya mazingatio miongoni mwa hayo ni pamoja na;-

### F.1 Mfuko wa Maendeleo ya Viwanda

42. **Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Maendeleo ya Viwanda (Industrial Development Fund) umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha uwekezaji na uzalishaji wa viwanda hapa

Zanzibar. Mfuko huu umeanza mwezi wa Septemba, 2024, hadi kufikia Machi, 2025, Mfuko huu umekusanya kiasi cha TZS 1.850 bilioni kutokana na vyanzo mbali mbali vya kodi za Serikali na zimetumika kwa ajili ya kuimarisha uwekezaji na uzalishaji wa Kiwanda cha Nguo cha Basra.

### F.2 Bima ya Lazima ya Safari kwa Wageni

**43. Mheshimiwa Spika,** Utoaji wa Huduma ya Bima ya Lazima ya Safari kwa Wageni (Mandatory Inbound Travel Insurance) ilikuwa na lengo la kuimarisha huduma kwa wageni wanaoingia Zanzibar na ilianza Oktoba, 2024. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha Dola za Marekani 20.03 milioni zimekusanywa kutokana na utekelezaji wa sera hii. Mapato yaliyokusanywa, yametumika kutekeleza huduma mbali mbali ikiwemo kuimarisha utoaji wa huduma za afya kwa wageni, kusafirisha maiti za wageni waliofia Zanzibar kutokana na sababu mbali mbali pamoja na malipo ya fidia ya upotevu wa pasi za kusafiria, malipo kwa waliopoteza mizigo yao wakati wa safari pamoja na kuwapandisha madaraja ya usafiri kwa wale abiria ambao hawakuweza kukaa katika madaraja ya chini kutokana na afya zao kuzorota wakati wakiwa safarini.

### F.3 Utekelezaji wa Bajeti Inayozingatia Jinsia na Usawa

**44. Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea na mageuzi ya Bajeti inayozingatia Jinsia na Usawa (Gender Responsive Budget) ili kuhakikisha usawa wa kijinsia unakwenda sambamba na dhana ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka 5 Zanzibar (ZADEP 2021-2026), utekelezaji wa Lengo Nambari 5 la Maendeleo Endelevu (SDGs) na Sera mbalimbali za sekta. Kwa mwaka 2024/2025, Serikali ilitenga kiasi cha **TZS 59.48 bilioni** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zinazozingatia jinsia na usawa kwa Wizara sita za majaribio ambazo ni; Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara

ya Afya, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora. Hadi kufikia Machi 31, kiasi cha **TZS 26.05 bilioni** zilitumika sawa na asilimia 44 ya fedha zilizopangwa.

**45. Mheshimiwa Spika,** Fedha hizo zilizotengwa zimetumika katika kutekeleza shughuli kuu zifuatazo:

i. Kushajihisha wanawake kusoma udaktari wa wanyama ambapo wanawake 11 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika kada hiyo nchini China,

ii. Kuanzishwa Vitalu 30 vya mbegu bora za mpunga vya wanawake katika bonde la Chaani, Kilombero kwa Unguja na Mlemele Pemba,

iii. Kupatiwa vifaa na mafunzo wakulima wa mwani 1,000 (wanawake 880, wanaume 120),

iv. Mafunzo ya muda mrefu kwa madaktari bingwa 21 wakiwemo madaktari 8 wa magonjwa ya kinamama na 11 wa masuala ya watoto,

v. Kutoa uelewa wa msaada wa huduma za kisheria, wanawake 280 wamefikiwa kwa Unguja na 499 kwa upande wa Pemba kati ya hao wanawake 167 wamepatiwa huduma za msaada wa kisheria,

vi. Mafunzo juu ya ushiriki wa wanaume katika malezi; Kanuni elekezi na Mifumo ya Usimamizi wa Familia katika Sheria; na Umuhimu wa Mawasiliano katika Malezi ya Watoto yamefanyika. Wanajamii 40 walishiriki mafunzo hayo wakiwemo wanawake 19 na wanaume 21, na

vii. Kupatikana kwa vifaa vya kike katika vyoo vya wanafunzi wanawake kutoka Skuli 123 mwaka 2023/2024 hadi kufikia Skuli 150 kwa kipindi cha Julai-Machi 2024/2025 sambamba na taulo za kike kwa wanafunzi 2,250 katika Skuli 150 Unguja na Pemba.

## G. MAFANIKIO YA SERIKALI KWA KIPINDI CHA JULAI 2024 HADI MACHI 2025

**46.** **Mheshimiwa Spika,** Naomba kwa uchache nieleze baadhi ya maeneo yaliyoelekezwa fedha na mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025;

i. **TZS 436.73 bilioni** zimetumika kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya miundombinu ya barabara, bandari na uwanja wa ndege,

ii. **TZS 159 bilioni** zimetumika katika sekta ya elimu na afya, na

iii. Kwa kipindi cha Miezi Tisa **TZS 28.9 bilioni** zimetumika katika sekta ya Maji na Uimarishaji wa upatikanaji wa Umeme.

**47.** **Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi hichi ni haya yafuatayo:

### a. Uimarishaji wa Ulinzi na Usalama na Upatikanaji wa Haki

**48.** **Mheshimiwa Spika,** Katika jitihada za Serikali za kuimarisha ulinzi na usalama na upatikanaji wa haki hadi kufikia Machi, 2025, kiasi cha **TZS 26.1 bilioni** zimetumika zikiwemo; **TZS 17.4 bilioni** kwa ajili ya Mradi wa Uimarishaji wa Ulinzi na Usalama na **TZS 8.7 bilioni** Ujenzi wa Mahakama saba, tatu za Wilaya na nne za Mikoa.

### b. Miundombinu ya Elimu

49. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeimarisha miundombinu ya elimu ikiwemo kujenga madarasa mapya 420, kukamilisha madarasa 170 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi, ujenzi wa dakhalia katika Skuli 11 na ujenzi wa ukuta wa Skuli ya Hasnuu Makame hadi kufikia Machi 2025, **TZS 147.8 bilioni** zimetumika.

### c. Miundombinu ya Barabara

50. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha miezi tisa, Serikali imetumia kiasi cha TZS 114.47 bilioni kwa ajili ya miundo mbinu ya Barabara. Matumizi hayo yameelekezwa katika maeneo yafuatayo;

    i. **TZS 11.9 bilioni** kukamilisha kilomita 42.95 za barabara kuu kwa kiwango cha lami, zikiwemo Jozani – Charawe - Ukongoroni, Fuoni - Tunguu, barabara ya Bungi na barabara za Nungwi.

    ii. **TZS 102.57 bilioni** ujenzi wa kilomita 95.79 ambapo kilomita 38.35 zimejengwa kwa kiwango cha lami ikiwemo; Micheweni-Shumba Mjini- Bandarini, Ukutini-Mtangani-Bandarini, Micheweni- Kiuyu-Maziwa Ng'ombe, Donge Mbiji - Chechele na Mwakaje – Mwachealale – Bumbwisudi na kilomita 57.44 zipo katika hatua ya kuweka kifusi zikijumuisha barabara za Chanjamjawiri – Pujini, Konde – Msuka na Masingini - Kijichi.

### d. Sekta ya Fedha

51. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya fedha ni muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi. Sekta hii inajumuisha huduma za Mabenki, Bima, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Soko la Mitaji na Dhamana, Mifumo ya malipo na huduma Ndogo za Fedha (Microfinance).

- **Sekta Ndogo ya Benki**

**52.** **Mheshimiwa Spika,** Sekta hii inajumuisha; Benki za biashara, Mawakala wa huduma za kibenki na mitandao ya simu. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, sekta hii iliendelea kuimarika na kuchangia kwa wastani wa asilimia 4.1 katika ukuaji wa Pato la Taifa la Zanzibar.

- **Amana**

**53.** **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi, 2025, amana katika benki zilizopo ziliongezeka hadi kufikia TZS 3,021.2 bilioni kutoka TZS 2,183.9 bilioni zilizokuwepo kipindi kama hicho mwaka 2024. Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ilikuwa na asilimia 53.3 ya amana zote; ikifuatiwa na benki za NMB, CRDB, NBC, na ABSA ambazo kwa pamoja zilichangia asilimia 33.2 ya amana zote hapa Zanzibar.

- **Wakala wa Huduma za Kibenki**

**54.** **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia mwezi Machi 2025, idadi ya benki zilizokuwa zikitoa huduma zilikuwa 14, na matawi ya benki 43, (Pemba matawi 10 na Unguja matawi 33), idadi ya mawakala wa benki (agent banking) ilikuwa 6,379 ambao ni asilimia 4.4 ya mawakala wote nchini Tanzania. Pemba kulikuwa na mawakala 2,999 na Unguja mawakala 3,380.

- **Huduma za Bima Zanzibar**

**55.** **Mheshimiwa Spika,** Hali ya Soko la Bima kwa upande wa Zanzibar inazidi kuimarika. Biashara ya bima imekua na kufikia asilimia 271, hii imetokana na mikakati mbalimbali ya Serikali ikiwemo;

i. Kuazishwa Sera ya Bima ya Lazima kwa Wageni wote wanaofika Zanzibar (Inbound Travel Insurance) yenye lengo la kutoa kinga dhidi ya majanga na dharura pindi yakitokea ndani ya siku tisini na mbili (92),

ii. Kuongeza wigo wa Biashara ya Bima kwa kufanya mashirikiano ya kimkakati na Makampuni na Mabenki mbalimbali katika mfumo wa (Bancassurance) kama vile (VodaBima, Mix by Yas Bima, Shirika la Posta Tanzania, NMB Bank, CRDB Bank, EXIM Bank, TCB Bank, DCB Bank, NBC Bank, BOA Bank, Mwalimu Commercial Bank, MUKOBA Bank na PBZ Bank),

iii. Kuanzishwa kwa aina mpya za bidhaa za bima kwenye soko la bima ili kukidhi mahitaji ya wananchi hususan wa kipato cha chini. Miongoni mwa hizo ni; huduma za bima kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo na wa kati na bidhaa za kilimo na uvuvi, na

iv. Matumizi ya bima kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kulinda majengo ya Umma, Magari ya Serikali, Bima ya Afya na Miradi ya maendeleo.

- **Malipo ya wahanga wa Ufilisi wa iliyokuwa Benki ya FBME**

56. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa wateja wa iliyokuwa benki ya FBME Serikali kwa kushirikiana na Bodi ya Bima ya Amana (DIB) tayari imeshalipa kiasi cha **TZS 5.423 bilioni** kwa wateja 564 malipo ya awamu ya kwanza ya asilimia 30% ya amana kwa kila mdai. DIB inaendelea kulipa awamu ya pili ya asilimia ishirini na tano (25%) na wateja **757** wanatarajiwa kulipwa kiasi cha **TZS 5.205 bilioni** katika awamu hii, huku hatua nyengine zikiendelea kuhakikisha amana zote za wateja zinalipwa.

**d. Uendeshaji wa Mashirika ya Umma**

57. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2024, hadi Machi 2025 kumekuwa na mafanikio makubwa katika uendeshaji wa Mashirika ya Umma yakiwemo;

i. Ukodishaji wa Bohari Kuu ya kuhifadhia bidhaa za Mafuta ya Nishati iliyopo Mtoni Unguja kwa Kampuni ya GBP Energies Limited Zanzibar,
ii. Kuanzishwa kwa Mfumo wa Usajili na Usimamizi wa Mali za Umma (ZGAMIS), jumla ya Mali za Umma zilizosajiliwa zimefikia 23,638 zenye thamani ya TZS 262 bilioni zikiwemo Majengo 153, Vyombo vya Moto 603, Vifaa vya TEHAMA 3,889, samani 17,579, Ardhi 29, na Mashine na Vifaa 1,218,
iii. Kuanzishwa kwa Mfumo na Muongozo wa Uondoaji wa Mali za Umma, na
iv. Kuanzishwa kwa Jukwaa la kwanza la wakuu wa Taasisi Zanzibar kwa lengo la kubadilishana uzoefu wa kiuongozi kwa sekta za umma na binafsi.

### e. Mashirikiano ya Kikanda na Kimataifa

**58. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha miezi tisa mashirikiano ya kiuchumi na kidiplomasia kwa SMZ na nchi mbalimbali kitaifa na kimataifa yamezidi kuimarika, kumekuwa na mahusiano kupitia ushiriki wa matamasha na makongamano ya ndani na nje ya nchi. Mheshimiwa Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amekuwa akishiriki katika masuala muhimu yakiwemo ya Siasa, Uchumi, Jamii, Diplomasia na Uwekezaji, Miongoni mwao ni;-

i. Kuhudhuria Maonesho ya 7 ya Kimataifa ya Uagizaji Bidhaa ya China (CIIE) yaliyofanyika Shanghai. Maonesho haya, yenye kaulimbiu **"Enzi Mpya, Mustakabali wa Pamoja"**, yalilenga kukuza biashara na uwekezaji kati ya China na nchi nyingine, ikiwemo Tanzania,
ii. Kuongoza Warsha maalum ya kukuza uwekezaji, utalii na Biashara kwa kushirikiana na Ubalozi wa China nchini Tanzania, kuhusu uimarishaji wa ushirikiano

wa kiuchumi na uwekezaji katika sekta za Viwanda, Kilimo, na Utalii,

iii. Kufanya ziara nchini Msumbiji kwa mwaliko wa Rais wa Msumbiji, Mheshimiwa Filipe Jacinto Nyusi. Lengo ni kuimarisha ushirikiano kati ya Zanzibar na Msumbiji na kufungua Milango ya ushirikiano zaidi katika sekta za Biashara, Uwekezaji, Uchukuzi, na Mawasiliano,

iv. Kufanya ziara nchini Indonesia. Mkutano wa Pili wa Jukwaa la Indonesia na Afrika, ambapo walijadili juu ya Ushirikiano wa kimkakati katika Ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani. Bandari hiyo itaunganisha huduma za uhifadhi wa nafaka, makontena, bandari kavu, chelezo, pamoja na hifadhi ya mafuta, ikiwa na lengo la kuwa “Trans-shipment Port” kwa ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika, ziara hii imeimarisha uhusiano kati ya Zanzibar na Indonesia, hususan katika sekta za uchumi wa buluu, usafirishaji, biashara, na viwanda, huku ikifungua milango ya ushirikiano wa kimkakati kwa maendeleo ya Zanzibar,

**59. Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliweza kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Majadiliano ya Kimkakati (Strategic Dialogue), uliofanyika katika Hotel ya Sea Cliff iliyopo nje kidogo ya mji wa Zanzibar. Lengo Kuu la Mkutano huo ilikuwa kuangalia juu ya namna bora ya Serikali na Washirika wa Maendeleo wanavyoweza kushirikiana kupitia Mpango wa Maendeleo wa Ushirikiano “Development Cooperation Framework (DCF)”.

## H. MAFANIKIO YA SERIKALI KWA KIPINDI CHA MUHULA WA KWANZA WA AWAMU YA NANE

**60. Mheshimiwa Spika,** Serikali za awamu zote zilizopita, zimekuwa zikifanya jitihada kubwa za kutekeleza mkakati juu ya mabadiliko ya kiuchumi sambamba na kuimarisha

ustawi wa raia. Kila awamu imekuwa na muendelezo na mabadiliko ya kipekee kulingana na utekelezaji wa Ilani na Ahadi zinazotolewa.

61. **Mheshimiwa Spika,** Awamu ya Kwanza ya Marehemu Mzee Abeid Amaan Karume, Rais wa Kwanza wa Zanzibar, mara baada ya Mapinduzi ya Mwaka 1964 alifanya mageuzi makubwa ya kiuchumi, kisiasa na kijamii katika kila nyanja. Miongoni mwa hayo ni pamoja na, Ujenzi wa Bandari, Uwanja wa Ndege wa Abeid Amaan Karume na Viwanja vya michezo ikiwemo Uwanja wa Amaan na Mao Tse Tung. Vile vile alianzisha Hospitali ya Mnazi Mmoja, Ujenzi wa Nyumba za Makaazi bora ya wananchi (Michenzani, Kikwajuni kwa Mjerumani, Mpapa, Makunduchi, Madungu na Wete). Alitangaza elimu bila malipo na kuasisi Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, huku akibeba ajenda kuu ya ***Kusimamia ufanyaji kazi kwa Uadilifu, Uzalendo na Uhuru bila ya Upendeleo.***

62. **Mheshimiwa Spika,** Awamu ya Pili ya Marehemu Aboud Jumbe Mwinyi nae amefanya mengi yakiwemo; Kuanzisha Chombo cha Kutunga Sheria ambacho ni Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Katiba ya Mwanzo ya Zanzibar ya Mwaka 1984, sambamba na kutunga na kusimamia Sera ya Usalama wa Chakula (food security) kwa kuanzisha mashamba ya kilimo ambayo yalikuwa na lengo la kuifanya Zanzibar kujitosheleza kwa chakula.

63. **Mheshimiwa Spika,** Awamu ya tatu ya Marehemu Alhaji Ali Hassan Mwinyi nayo ilikuja na mageuzi makubwa ya uchumi kwa kuruhusu sekta binafsi kushiriki katika utoaji wa huduma za uzalishaji pamoja na biashara kupitia soko la uchumi huria hali iliyopelekea kupewa jina la ***Mzee Ruksa*** huku akibeba ujumbe mzito na maarufu wa ***Zanzibar Ni Njema Atakae na Aje.***

**64. Mheshimiwa Spika,** Awamu ya Nne ya Marehemu Idrissa Abdul Wakil ilisimamia uanzishwaji wa viwanda vidogovidogo kwa kuanzisha viwanda vya utengezaji nyaya za umeme, viwanda vya kutengeneza vyombo, nguo na kuendeleza kilimo na ujumbe wake mkubwa kwa wakati wake ulikuwa ***Mtakula***.

**65. Mheshimiwa Spika,** Awamu ya tano ya Dkt Salmin Amour Juma, ilidhamiria kuimarisha Sekta ya Utalii ili sekta hii iwe ndio sekta kiongozi kwa uchumi wa Zanzibar badala ya zao la Karafuu ambalo bei iliporoka katika soko la dunia kutokana na kuwa na wazalishaji wengi. Vile vile Dkt. Salmin aliimarisha na kuhamasisha uwekezaji kwa kuanzisha maeneo huru ya uwekezaji (yakiwemo Fumba na Amani). Katika awamu hii, taasisi kadhaa zilianzishwa zenye mnasaba wa kuifungua Zanzibar kiuchumi zikiwemo; Mamlaka ya Uwekezaji na Ukuzaji Uchumi Zanzibar, Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF). Kipindi hiki Soko la Biashara la Zanzibar lilikuwa limeshamiri kwa wafanya biashara kutoka Comoro na Tanzania Bara hali iliyopelekea Zanzibar kuitwa ***"Dubai ndogo".***

**66. Mheshimiwa Spika,** Katika Awamu ya Sita ya Dkt. Amani Abeid Karume, Serikali iliimarisha mawasiliano na miundombinu, Marekebisho ya Katiba ya Zanzibar ambayo yalipelekea Maridhiano ya Kisiasa na kuanzishwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Kipindi cha awamu hii, Serikali iliunganisha Umeme wa Submarine Cable uliopita chini ya bahari na kukamilisha ujenzi wa Nyumba za Michenzani block namba 9 na 10.

**67. Mheshimiwa Spika,** Awamu ya Saba ya Dkt Ali Mohamed Shein, Serikali, ilijikita katika kufanya mageuzi ya utendaji kazi na Maslahi ya Umma, ilianzisha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi (ZAECA), iliimarisha

Makaazi Bora ya Wananchi kwa kuanza na kukamilisha ujenzi wa Nyumba za Makaazi Kwahani, Nyumba za ZSSF Mbweni, Michenzani Mall na Mnara wa Kisonge. Katika kipindi hichi pia, kulifanyika mapitio pamoja na kukamilisha na kuzindua Dira ya Maendeleo ya 2050, kuanza kwa Sera ya Uchumi wa Buluu, malipo ya Pencheni Jamii kwa wazee waliofikisha umri wa miaka 70 pamoja na mageuzi makubwa ya kauli mbiu ya **Tuache Kufanya Kazi kwa Mazoea**.

**68.** **Mheshimiwa Spika,** Awamu ya nane, chini ya uongozi wa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, imekuja kuimarisha zaidi yale yote yaliyotekelezwa katika awamu zote saba zilizotangulia. Licha ya changamoto za hali ya uchumi na bajeti katika kipindi cha mwaka 2020/2021, kutokana na athari za maradhi ya UVIKO -19 ambayo yaliathiri uchumi wa nchi nyingi ikiwemo Zanzibar, kwa imani, ujasiri na shauku ya kuwaletea Maendeleo Wazanzibari kupitia Kauli Mbiu yake **"Yajayo Neema Tupu"** nchi haikuyumba na ikaendelea kupiga hatua katika sekta mbali mbali.

**69.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha miaka minne, hali ya kiuchumi Zanzibar imezidi kuimarika, nchi imeongeza haiba nzuri kupitia kuimarisha miundombinu ya barabara, mifumo ya TEHAMA pamoja na utendaji kazi katika sekta za afya, elimu na huduma za maji safi na salama, ujenzi na uimarishaji wa Ofisi za Serikali, miundombinu ya michezo pamoja na ujenzi wa masoko mapya ya kisasa.

**70.** **Mheshimiwa Spika,** Naomba uniruhusu kuwasilisha kwa muhtasari tu mafanikio ya utendaji ya Serikali ya Awamu ya Nane, kwani haiwezekani kuyataja yote kwa ukamilifu wake hata tukiandika kurasa zaidi ya 100 hatutaweza kufikia hata robo ya yale yaliyokwisha kutekelezwa. Miongoni mwa hayo ni;-

### a. Ongezeko la Bajeti na Matumizi Halisi ya Serikali

**71. Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Serikali imeongezeka kutoka **TZS 1,579.2 bilioni** 2020/2021, hadi kufikia **TZS 5,182.89 bilioni** kwa Mwaka 2024/2025, sawa na ongezeko la asilimia **228.2**.

i. Bajeti ya Miradi ya Maendeleo imeongezeka kutoka **TZS 609.80 bilioni** Mwaka 2020/2021 hadi kufikia **TZS 3,271.11** bilioni Mwaka 2024/2025.

ii. Bajeti ya matumizi mengineyo kutoka **TZS 969.30 bilioni** Mwaka 2020/2021 hadi kufikia **TZS 1,911.79 bilioni** Mwaka 2024/2025.

iii. Kwa kipindi cha miaka minne, Serikali imefanikiwa kupokea Mikopo na Misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kiasi cha **USD 1,786.40 milioni** sawa na **TZS 4.876 trilioni** kwa ajili ya kugharamia miradi mbali mbali ya maendeleo na ya kimkakati.

**72. Mheshimiwa Spika,** Kumekuwa na ongezeko kubwa la makusanyo halisi ya mapato ya ndani kutoka **TZS 781.01 bilioni** Mwaka 2020/2021 hadi **TZS 2,130.79 bilioni** 2023/2024 sawa na ukuaji wa asilimia **172.8**.

**73. Mheshimiwa Spika,** Matumizi Halisi ya Miradi ya Maendeleo yameongezeka kutoka **TZS 213.71 bilioni** Mwaka 2020/2021, hadi **TZS 1,407.10 bilioni** kwa mwaka 2023/2024 sawa na ukuaji wa asilimia **558**.

**74. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi ya kawaida yameongezeka kutoka **TZS 740.11 bilioni** hadi kufikia **TZS 1,234.87 bilioni**, sawa na ukuaji wa asilimia 66 hii inaonesha mabadiliko makubwa yaliyofanywa na Serikali kuelekeza zaidi matumizi kwenye Miradi ya Maendeleo.

75. **Mheshimiwa Spika,** Kutokana na ongezeko hilo la Bajeti, Matumizi Halisi yamekuwa yakiongezeka na kupelekea mafanikio makubwa katika utekelezaji wa Bajeti za Kisekta na hivyo kuweza kuchangia Uchumi na Kuimarisha Utoaji wa Huduma za jamii ikiwa ni jukumu la msingi la Serikali; Miongoni mwa Wizara hizo ni;-

i. Matumizi halisi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa fedha za ndani kutoka **TZS110.784 bilioni**, Mwaka 2020/2021 hadi kufikia **TZS 428.956 bilioni**, Mwaka 2023/2024.

ii. Matumizi halisi ya Wizara ya Afya kwa fedha za ndani kutoka **TZS 28.023 bilioni**, Mwaka 2020/2021 hadi kufikia **TZS 163.427 bilioni**, Mwaka 2023/2024.

iii. Matumizi halisi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na uchukuzi kwa fedha za ndani kutoka **TZS 35.560 bilioni**, Mwaka 2020/2021 hadi kufikia **TZS 448.566 bilioni**, Mwaka 2023/2024.

iv. Matumizi halisi ya Wizara Uchumi wa Buluu na uvuvi kwa fedha za ndani kutoka **TZS 7.591bilioni**, Mwaka 2020/2021 hadi kufikia T**ZS 15.273 bilioni**, Mwaka 2023/2024.

v. Matumizi halisi ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa fedha za ndani kutoka TZS 1.759 bilioni, Mwaka 2020/2021 hadi kufikia **TZS 7.694** Mwaka 2023/2024.

vi. Matumizi halisi ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, maliasili na Mifugo kwa fedha za ndani kutoka **TZS 37.476 bilioni**, Mwaka 2020/2021 hadi kufikia **TZS 57.597 bilioni**, Mwaka 2023/2024.

76. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kwa ufupi nielezee mafanikio ya utekelezaji wa sekta mbali mbali kama ifuatavyo:

**b. Sekta ya Mawasiliano**

77. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kuimarisha miundombinu ya mawasiliano kwa kulaza Mkonga wa Taifa wa mawasiliano kutoka kilomita 450 kwa Mwaka 2021/2022 hadi kufikia kilomita 1,500 kwa Mwaka 2024/2025. Lengo ni kuhakikisha kuwa huduma za mawasiliano ikiwemo huduma za mtandao zinapatikana kwa urahisi Unguja na Pemba ili kukuza uchumi wa kidigitali Zanzibar.

78. **Mheshimiwa Spika,** Shehia zote 388 zilizopo Unguja na Pemba zimepatiwa Anuani za Makaazi zipatazo 528,417. Makaazi yote Unguja na Pemba yamesajiliwa katika Mfumo wa Anwani ya Makaazi na kutenga na kutangaza maeneo huru ya uwekezaji Kidigitali Zanzibar (Zanzibar Digital Free zone) yaliyopo Fumba ambapo Serikali itajenga Mji wa TEHAMA (Zanzibar Cyber City).

- **Usafiri wa Anga na Baharini**

79. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha miaka minne, Serikali imetumia kiasi cha TZS 445.914 bilioni kwa ajili ya kuimarisha huduma za Anga na Bandari zikiwemo (TZS 154.570 bilioni kwa ajili ya kuimarisha huduma za Usafiri wa Anga Unguja na Pemba na TZS 291.344 bilioni kwa uimarishaji wa sekta ya usafiri wa baharini. Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni;

i. Kuanza rasmi Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba, ambao utaongezwa urefu wa barabara ya kuruka na kutua ndege (runway and taxi way). Kujenga jengo jipya la abiria (Terminal Building) na miundombinu husika itakayowezesha uwanja huo kutua ndege aina ya Code C (Boeing 737-800).

ii. Kuendelea na ujenzi wa Jengo la Abiria (Terminal II) lenye uwezo wa kuhudumia abiria 1,300,000 kwa mwaka.

iii. Kujenga ushirikiano na sekta binafsi nchini kwa kuingia mkataba na kampuni mbali mbali za kimataifa zikiwemo; ZMT/AGL Bandari ya makontena Malindi, MJ group Bandari ya Fumba na Mkoani na ZF Devco Bandari ya abiria Maruhubi na Malindi.

80. **Mheshimiwa Spika,** Mafanikio mengine katika huduma za usafiri wa Bahari ni katika maeneo yafuatayo;

i. Kuendelea na Ujenzi wa Bandari ya abiria Maruhubi kwa kushirikiana na Kampuni ya ZF DEVCO pamoja na Kampuni ya MJ kwa ujenzi wa gati katika Bandari ya Fumba,
ii. Kuimarisha Bandari ya Mkoani ikiwemo kutoa huduma za meli za makontena, kujengwa bandari kavu na kuweka baji kwa ajili ya boti za mwendo kasi,
iii. Kukamilisha Ujenzi wa Bandari ya Shumba Mjini Micheweni itakayowezesha safari baina ya Pemba, Mombasa na Tanga,
iv. Kukamilisha upembuzi yakinifu na master plan ya ujenzi wa bandari ya Wete, na
v. Kuanza ujenzi wa bandari ya Makontena Mangapwani.

- **Usafiri wa Nchi Kavu (Barabara)**

81. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara za lami. Kiasi cha **TZS 565.818 bilioni** zimeshatumika na kufanikiwa kufikia kilomita 1,023.37 mwaka 2024/2025 kutoka kilomita 815.45 mwaka 2021/2022, zikiwemo barabara za ndani, barabara za mijini na barabara kuu Unguja na Pemba. Katika kipindi cha miaka minne, Serikali imefanikiwa kujenga kilomita 321.295 za barabara kwa kiwango cha lami Unguja na Pemba. Kati ya hizo kilomita 23.8 ni barabara kuu, kilomita 80 barabara za mijini na kilomita 217.495 ni barabara za ndani na vijijini.

82. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya kilomita 448.28 za barabara za kiwango cha lami Zanzibar, zinaendelea kujengwa na zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**c. Kuimarika kwa Huduma za Kijamii**

- **Sekta ya Afya**

83. **Mheshimiwa Spika,** Katika uimarishaji wa Miundombinu ya Afya katika ngazi zote za utoaji wa huduma, Serikali imefanikiwa kuimarisha maeneo yafuatayo;

i. Ujenzi wa nyumba za makaazi za Wafanyakazi zinazo hudumia familia 76 katika Hospitali ya Rufaa ya Abdulla Mzee-Mkoani Pemba zenye thamani ya TZS 16.481bilioni na ujenzi wa vyumba vya wagonjwa mahututi (ICU) kwa thamani ya TZS 0.828 bilioni,

ii. Ujenzi na ununuzi wa vifaa tiba na utoaji wa huduma kwa Hospitali 10 za Wilaya (Unguja ni Ijitimai, Chumbuni, Mbuzini, Mwera Pongwe, Kitogani, Pangatupu na Kivunge na Pemba ni Micheweni, Kinyasini na Vitongoji) na hospitali ya Mkoa – Lumumba, kwa thamani ya TZS 104.440 bilioni zikiwemo (TZS 92.678 bilioni gharama za ujenzi na TZS11.762 bilioni ununuzi wa vifaa tiba),

iii. Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika hospitali ya Mwera Pongwe, Kitogani na Pangatupu kwa Unguja na upande wa Pemba Hospitali ya Kinyasini na Vitongoji zenye thamani ya **TZS 20.402 bilioni**,

iv. Ujenzi wa vituo vya afya 11 (Health Centers) (Magomeni Wandaras, Sebleni, Tunguu, Kinduni, Nungwi, Kizimkazi na Tumbatu kwa Unguja na Pemba ni Konde, Chonga, Mtambile na Jadida). Kiasi cha TZS 42.742 bilioni zimetumika kutoka Serikalini,

v. Ujenzi wa maabara mpya ya kisasa ya Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar yenye viwango vya Shirika la Afya Duniani (WHO) ambapo mradi huu uligharimu **TZS 9.900 bilioni**,

vi. Ujenzi wa Tanuri mbili kubwa (High Tech Incinerators) za kuchoma taka za Hospitali (medical waste) eneo la Kibele kwa Unguja yenye uwezo wa kuchoma kilogramu 900 kwa saa na eneo la Vitongoji kwa upande wa Pemba lina uwezo wa kuchoma kilogramu 750 kwa saa, mradi huu umegharimu TZS 5.213 bilioni,
vii. Kupitishwa kwa Sheria Nambari 1 ya Mwaka 2023 ya kuanzisha Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF) na kuanza kutoa huduma ambapo hadi sasa wanachama 305,113 (63,563 wachangiaji na 242,814 wategemezi) wamesajiliwa.

**84. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha miaka minne Serikali imeajiri watumishi wapya wa sekta ya Afya 2,008 wa kada mbalimbali ikiwemo madaktari 487 sambamba na kufunguliwa rasmi kwa Jengo la Maabara ya Kujifundishia (Skill Laboratory) iliyopo katika eneo la Hospitali ya Mkoa–Lumumba.

- **Sekta ya Elimu**

**85. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha miundombinu na Ubora wa Elimu, Serikali imekuwa ikiongeza Bajeti ya sekta ya Elimu kutoka TZS 265.5 bilioni Mwaka 2021/2022 hadi kufikia TZS 830 bilioni kwa Mwaka 2024/25 sawa na ongezeko la asilimia 212.6 maeneo ambayo yamefanikiwa ni;-
i. Ujenzi wa Skuli mpya 35 za ghorofa zikiwemo Tumbatu, Kojani, Mfenesini, Kifundi, Konde, Maziwa ng'ombe na Tumekuja,
ii. Ujenzi wa dakhalia kutoka dakhalia sita Mwaka 2021/2022 hadi kufikia dakhalia 21 Mwaka 2024/2025 na Ununuzi wa seti 102,671 za viti na meza na kusambazwa katika Skuli za Unguja na Pemba pamoja na vitanda 1,246 kwa ajili ya dakhalia,

iii. Ununuzi wa vifaa vya TEHAMA, kompyuta za mezani 3,002, kompyuta mpakato 1,051, vishikwambi 6,193 na projekta 1,002,

iv. Utekelezaji wa mtaala mpya kuanzia ngazi ya elimu ya Maandalizi, Msingi na Sekondari ambapo vitabu **3,424,436** vya kufundishia na kujifunzia vimenunuliwa na kusambazwa katika Skuli za Unguja na Pemba. Kufuatia mtaala mpya Skuli 32 za Sekondari zimeanza kufundisha masomo ya amali,

v. Ufaulu wa wanafunzi wa vipawa na michepuo katika Mitihani ya Darasa la Saba umeongezeka kutoka asilimia 5.5 mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 11.34, hii imetokana na kuwepo mazingira mazuri zaidi ya kujifunzia na kufundishia na

vi. Kuongezeka kwa Bajeti ya Mikopo ya elimu ya juu kutoka TZS 11.5 bilioni hadi kufikia TZS 33.4 bilioni na idadi ya wanafunzi wanaopatiwa mikopo ya elimu ya juu imeongezeka kutoka wanafunzi 4,261 hadi kufikia wanafunzi 11,495.

**86. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha miaka minne Serikali imeajiri watumishi wapya wa sekta ya Elimu 3,531 wa kada mbalimbali ikijumuisha walimu 110 wa elimu mjumuisho.

- **Upatikanaji wa Huduma ya Maji Safi na Salama**

**87. Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kujenga, kukarabati, kusambaza mitandao ya maji, pamoja na kuimarisha usimamizi wa vyanzo vya maji nchini. Hadi Machi, 2025 hali halisi ya uzalishaji wa maji safi na salama nchini imefikia lita **211,106,767** (Unguja lita 154,808,220 na Pemba lita 56,298,547) kwa siku ambapo mahitaji halisi ya maji nchini ni lita **278,432,860** (Kisiwa cha Unguja ni lita 190,938,860 na Pemba lita 87,494,000). Mafanikio mengine ni pamoja na;-

i. Kiasi cha **TZS 246.03 bilioni** zimetumika kwa Utekelezaji wa Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar. Maeneo yaliyofanyiwa kazi ni pamoja na; uchimbaji wa visima (102), ukarabati wa visima (36), ununuzi na ufungaji wa pampu 51, uimarishaji na ubadilishaji wa mtandao chakavu kwa masafa ya kilomita 319, ujenzi na ukarabati wa matangi, ulazaji wa mabomba kwa kilomita 466.9 na ujenzi wa vibanda 51 vya kuhifadhia pampu kwa Unguja na Pemba,

ii. Kupatikana kwa huduma ya maji safi na salama katika Shehia 342 kati ya **Shehia 388** na kusambaza mitandao ya Maji Zanzibar. Aidha, Shehia 216 kati ya Shehia 260 zinanufaika na upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama Unguja, na kwa upande wa Pemba Shehia zote 128 zinafaidika na huduma ya maji safi na salama.

- **Sekta ya Nishati na Umeme**

**88. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea na jitihada za kuhakikisha Zanzibar inapata vyanzo vyake vya ndani vya uzalishaji umeme pamoja na kuwepo kwa miundombinu imara ya kusafirisha na kusambaza umeme. Katika kulifanikisha suala hilo, Serikali imefanikiwa kusaini Hati za Makubaliano (MoU) na Kampuni tofauti ili kuweza kukabiliana na changamoto za kisekta kama ifuatavyo:-

i. Kampuni ya Techsol Solution Limited (Mwakilishi wa Kampuni ya Von Boyyett Corporation and Energy Consortium) kutoka nchini Kenya. Kampuni hio ina lengo la kuzalisha Megawati 100 kwa kutumia nishati ya Gesi,

ii. Kampuni ya O & L Nexentury GmbH kutoka nchini Ujerumani. Kampuni hiyo ina lengo la kuzalisha Megawati 30 kwa kutumia nishati ya jua,

iii. Kampuni ya Aseel Oilfield Services kutoka nchini Uganda. Kampuni hiyo ina lengo la kuzalisha Megawati 20 kwa kutumia nishati ya upepo, na

iv. Kampuni ya Synotech kutoka nchini China ambayo ina lengo la kuzalisha Megawati 50 kwa kutumia Nishati ya jua.

**89. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) imefanikiwa kupunguza bei ya kuunganisha umeme kwa wananchi kwa wastani wa asilimia 50. Punguzo hilo ni kutoka **TZS 464,000** na kufikia **TZS 200,000** kwa gharama za uungaji usiozidi mita 30; kutoka TZS 1,700,000 kufikia TZS 690,000 kwa gharama za uungaji wa nguzo 1 na kutoka TZS 2,600,000 kufikia TZS 1,040,000 kwa gharama za uungaji wa nguzo mbili (2). Vile vile, Serikali imeingia mikataba na:

i) Kampuni ya Aseel Oil Fiel itakayozalisha umeme kwa kutumia Nishati ya Nguvu za Upepo (Wind Energy) ya kiwango cha Megawati mia mbili (200MW) katika eneo la Matemwe.

ii) Kampuni ya NextGen itakayozalisha umeme kwa kutumia nishati ya nguvu za Jua (Solar Energy) ya kiwango cha megawati thelathini (30MW) pamoja na uhifadhi wa umeme huo (Battery Storage) kwa kiwango cha megawati themanini kwa saa (80MWh).

**e. Uchumi wa Buluu**

**90. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Uchumi wa Buluu mafanikio yaliyopatikana ni;

i. Kuongezeka kwa kiwango cha uzalishaji wa Samaki kwa asilimia 107.2 kutoka tani 38,107 zenye thamani ya **TZS 205.35 bilioni** mwaka 2020 hadi kufikia tani 78,943 zenye thamani ya **TZS 618.18 bilioni** mwaka 2024.

ii. Uzalishaji wa zao la Mwani umeongezeka kwa asilimia **124.6** kutoka tani 8,785 zenye thamani ya **TZS 5.387** bilioni mwaka 2020 hadi kufikia tani 19,716 zenye thamani ya **TZS 16.14 bilioni** mwaka 2024.

- **Mafuta na Gesi Asilia**

**91. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia ZPRA imetekeleza yafuatayo;

i. Kutangaza vitalu 10 vya Mafuta na Gesi Asilia (8 Baharini na 2 nchi kavu kwa wawekezaji kupitia majukwaa na mikutano mbali mbali ya kimataifa,

ii. Kukamilisha uwekaji wa miundombinu ya usimamizi wa taarifa za Mafuta na Gesi Asilia ikiwemo ujenzi wa kituo maalumu cha kuhifadhia na kukagulia taarifa za Mafuta na Gesi Asilia pamoja na ununuzi wa vifaa vinavyohusika na uhifadhi wa taarifa hizo.

**f) Uwekezaji**

**92. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha mazingira mazuri ya uwekezaji katika kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya Mwaka 2050 na kukuza uchumi, Serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji wa ndani na nje ili kuchochea maendeleo ya sekta.

**93. Mheshimiwa Spika,** Zaidi ya nchi 20 wamewekeza nchini, wakiongozwa na mataifa ya UAE, China, India na Oman. Serikali katika kuhakikisha kunakuwa na ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya uwekezaji maeneo kadhaa yameboreshwa yakiwemo;-

i. Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP) ilitungwa mwaka 2021, na sasa inatumika kama msingi wa kisheria wa kuendeleza miradi mikubwa,

ii. Kituo cha Huduma kwa Mwekezaji (One Stop Centre) kimeimarishwa ambapo muda wa kusajili miradi ya uwekezaji umepungua kutoka siku 30 hadi siku 7,
iii. Kuanzisha Mfumo wa Kielektroniki wa kuwahudumia Wawekezaji ambao umerahisisha utoaji wa huduma kwa kupunguza muda na urasimu katika kuwahudumia wawekezaji nchini,
iv. Kuandaa taarifa fupi za miradi (Project Profile) zaidi ya 70, kwa lengo la kuwarahisisishia wawekezaji kupata taarifa za miradi yenye tija inayopendekezwa na Serikali kutekelezwa kwa manufaa ya Umma,
v. Kutangaza Visiwa 21 kwa awamu ya kwanza kwa ajili ya uwekezaji na tayari visiwa 15 vimepata wawekezaji, ambapo dola za kimarekani Milioni 384 zinatarajiwa kuwekezwa katika miradi hiyo. Kati ya Visiwa hivyo, Visiwa Tisa viko katika hatua tofauti za ujenzi na kisiwa cha Bawe na Changuu vimeshaanza kutoa huduma,
vi. Kuendelea na Ujenzi wa "logistic Parks" katika eneo lenye ukubwa wa hekta 4.5 katika eneo Huru la Uchumi la Uwanja wa Ndege wa AAKIA unaokusudia kujenga jumla ya maghala 20 kwa awamu tofauti. Maghala mawili (2) yenye ukubwa wa mita (45 urefu x 25 upana) yamekamilika, na
vii. Kuweka vivutio kwa Wawekezaji Wenye Asili ya Tanzania (Diaspora) wenye viwanda na Vivutio Maalum kwa wawekezaji wa Kimkakati (strategic Investors) kwa mujibu wa Sheria ya Uwekezaji namba 10 ya mwaka 2023.

- **Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

**94. Mheshimiwa Spika,** Maendeleo ya kweli lazima yawe jumuishi, yanayowagusa wananchi wa ngazi zote. Serikali kupitia Taasisi za Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi, imechukua hatua mbalimbali kuwawezesha vijana na wanawake ambao ndio nguvu kazi ya Taifa zikiwemo;

i. Serikali kupitia Taasisi za Fedha, imerahisisha upatikanaji wa mitaji ambapo mikopo yenye thamani ya **TZS 21.5 bilioni** ilitolewa kwa wajasiriamali,
ii. Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar (ZEEA) umetoa mikopo ya **TZS 890.575 milioni** (Unguja 535,175 na Pemba 355,400 milioni) kwa wananchi 4,855, Unguja ni 2454 (wanaume 1188 na wanawake 1266) na Pemba 2401 (wanaume 916 na wanawake 1485),
iii. Kupitia Programu ya INUKA (fedha za ahuweni ya UVIKO-19), Serikali imetoa mikopo ya **TZS 34.295 bilioni** (Unguja TZS 24.028 bilioni na Pemba 10.267 bilioni) kwa wananchi 22,025 Unguja ni 12,018 (wanaume 4,838 na wanawake 7,180) na Pemba 10,007 (wanaume 4,105 na wanawake 5,902),
iv. Programu ya makundi maalum ya Wajasiriamali (4.4.2) imetoa mikopo ya **TZS 1.317 bilioni** (Unguja TZS 620.398 milioni na Pemba 697.505 milioni) kwa wananchi 1,518 Unguja ni 943 (wanaume 115 na wanawake 828) na Pemba 575 (wanaume 95 na wanawake 480),
v. Programu ya Uwezeshaji kutoka Mfuko wa Abudhabi imetoa mikopo ya **TZS 3.584 bilioni**,
vi. Programu ya Vifaa vya Nyuki, imetoa mikopo ya **TZS 247.566 milioni** (Unguja 128,960,000 na Pemba 118,606,000) kwa wananchi 1,704 Unguja na Pemba 941.

- **Ajira**

**95. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha miaka 4, Serikali imefanikiwa kutoa ajira 233,615 kupitia sekta rasmi na zisizo rasmi. Kati ya ajira hizo sekta rasmi 157,789 na sekta zisizo rasmi 75,826 (wanaume 116,476 na wanawake 117,139). Sehemu zilizochangia zaidi uzalishaji wa ajira ni: Mahoteli, Skuli Binafsi, Hospitali Binafsi, Kampuni za Mawasiliano, Ujenzi, Vituo vya mafuta na katika Taasisi Zisizo za Kiserikali.

Sambamba na ajira hizo, Serikali pia ilisaidia watu kujiajiri wenyewe kwa kuwapatia mtaji kupitia mfuko wa Uwezeshaji na Programu ya ajira kwa Vijana kwa Mkopo nafuu.

**96.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa ajira ya sekta ya umma, Serikali imeajiri takriban watumishi 16,466 katika kada mbalimbali.

### g) Maendeleo ya Sekta ya Ardhi na Makaazi

**97.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali imepata mafanikio kadhaa katika kusimamia na kuendeleza Sekta za Ardhi na Makaazi bora kwa jamii, yakiwemo;

i. Kufanya utambuzi wa maeneo 13 na viwanja 6,435 vimefanyiwa uhakiki na kutambuliwa katika maeneo ya Shakani, Meya, Mbweni na Jambiani kwa Unguja na Gombani, Utaani na Konde Pemba,

ii. Kupanga na kupima maeneo 8 kwa ajili ya nyumba za makaazi ya wananchi ikiwemo (Finya, Ziwani na Mfikiwa kwa upande wa Pemba, Kibele, Kisakasaka, Chumbuni, Chuini na Matemwe kwa upande wa Unguja), na

iii. Kuandaa Mpango wa matumizi ya ardhi za akiba katika zoni tano (5). Zoni ya Kaskazini katika maeneo ya Matemwe (Kikadini, Jugakuu, Kijini na Kigomani), Zoni ya Kusini (Kitogani, Paje, Jambiani, Makunduchi na Kizimkazi), Zoni ya Mjini Magharibi (Fumba, Chuini na Masingini), Zoni ya Kaskazini Pemba (Makangale, Konde, Msuka na Chamanangwe) na Zoni ya Kusini Pemba (Tibirinzi, Wesha na Chambani).

- **Sekta ya Makaazi**

**98.** **Mheshimiwa Spika,** Katika sekta ya Makaazi Serikali imefanikiwa kutekeleza yafuatayo: -

i. Kukamilisha ujenzi wa nyumba za makaazi 72 za Mombasa kwa Mchina Unguja kiasi cha **TZS 9.5 bilioni** zimetumika,

ii. Kiasi cha TZS 151 bilioni zinatarajiwa kutumika kwa ujenzi wa nyumba 3,000 katika eneo la Chumbuni. Awamu ya kwanza ya mradi huo utahusisha ujenzi wa nyumba 1,095,

iii. Kufanya Usajili wa Umiliki wa Fleti 591 katika Nyumba za Maendeleo Kilimani, Michenzani, Kikwajuni, Mombasa kwa Mchina, Machomane, Ng'ombeni, Uweleni na Mapinduzi.

**h) Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira**

**99. Mheshimiwa Spika,** Katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kutekeleza programu za uhifadhi na usimamizi wa mazingira. Hatua hizo ni pamoja na kujenga ukuta ili kuzuia athari zinazoletwa na maji ya bahari katika makaazi na mashamba ya wananchi katika maeneo ya Msuka Kaskazini Pemba, Wilaya ya Micheweni, Likoni kuelekea Kojani Wilaya ya Wete, Kisiwa Panza Wilaya ya Mkoani na Ujenzi wa tuta katika eneo la Tovuni Wilaya ya Wete Pemba. Kiasi cha **TZS 1.125 bilioni** zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa kuta katika maeneo mbali mbali kupitia Mradi wa Uhimili wa Athari Za Mabadiliko ya Tabianchi.

**i) Maendeleo ya Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale**.

**100. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Miaka 4, Serikali imeendelea kujikita katika kukuza Sekta ya Utalii na kuhifadhi urithi wa kihistoria kama mihimili ya uchumi wa Taifa, huku ikitekeleza miradi inayochochea maendeleo na kuongeza mchango wa sekta hizi katika pato la taifa.

101. **Mheshimiwa Spika,** Maeneo ambayo yamepata mafanikio ni pamoja na;

i. Kuongeza matamasha ya kutangaza utalii nchini kutoka 3 hadi kufikia 8. Tamasha la Uwekezaji na Utalii. Fahari ya Zanzibar, Tamasha la Vyakula vinavyopandwa bila ya kutumia mbolea au viuatilifu vya kemikali yaani "Organic". Tamasha la Kizimkazi, Zanzibar Holiday Market Festival, Trace Music Awards, Halal Tourism Festival, Tamasha la Vyakula vya Asili (Makunduchi) na Tamasha la Utalii na Utamaduni (Pemba Tourisport Bonanza and Culture).

ii. Uwekezaji katika Sekta ya Utalii umeongezeka kutoka miradi ya kitalii 995 iliyosajiliwa katika mwaka 2020 hadi kufikia miradi 1,695 mwaka 2024.

iii. Kuandaa mashindano ya michezo ya kimataifa kama mashindano ya "kite surfing" Mbio za "Marathon", Michezo ya "Triathlon", "Beach Soccer," na "Beach Volleyball", yamechangia kuvutia watalii zaidi, hali hii imepelekea ongezeko kubwa la watalii nchini.

iv. Kupitia Filamu ya The Royal Tour na Presidential Tour, ambazo ziliwahusisha Marais wa Tanzania na Zanzibar, zimekuwa nyenzo muhimu katika kuitangaza Zanzibar kimataifa.

v. Kushinda tuzo sita za kimataifa za utalii katika kipindi cha miaka mitano, ikiwemo 'Africa Tourism Board of the Year", "Africa's Leading Beach Destination", "4th Top Destination in Africa", "9th World Top Honeymoon Destination", "Best Romantic Destination" na "2nd Best Island Holidays" ambazo zimeongeza mvuto wa kimataifa kwa visiwa vya Zanzibar kama eneo bora la mapumziko na burudani.

102. **Mheshimiwa Spika,** Kwenye urithi wa kihistoria, Serikali kwa kushirikiana na Taasisi za elimu ya juu, imefanya tafiti za ekolojia kwa lengo la kufahamu kwa kina historia

ya sehemu husika kwa kuyarejesha kwenye hadhi yake ya kihistoria. Maeneo hayo ni eneo la kihistoria la Chwaka, Dunga, Kongwe, Mkokotoni pamoja na maeneo ya Kizimbani, Machui, Kombeni, Maungani, Jumbi, Kama, Bububu na Mwakaje. Tafiti hizi zimegundua mambo mengi ya kihistoria ambapo awali mambo hayo yalikuwa hayatambuliki.

103. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanikiwa kuimarisha uwekezaji katika maeneo ya kihistoria ambapo maeneo waliyopatiwa wawekezaji ni Fukuchani, Ngome Kongwe, Chuini, Maruhubi, Mahamamu ya Kijichi, Forodhani na Hamamni, Bustani za Mnazi Mmoja na Africa House. Hatua hii imeongeza thamani ya vivutio vya utalii wa kihistoria.

**j) Biashara na Viwanda**

104. **Mheshimiwa Spika,** Serikali katika jitihada za kuimarisha Biashara na Viwanda imefanikiwa kuboresha katika maeneo yafuatayo-;

i. Kujenga eneo la Maonesho ya Biashara huko Dimani, Wilaya ya Magharibi B,
ii. Kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi (Master Plan) ya eneo la Kituo Cha Kimataifa cha Biashara na Mikutano – MICE katika eneo la Dimani,
iii. Ujenzi wa kiwanda cha kusarifu Mwani kilichopo Chamanangwe Mkoa wa Kaskazini Pemba, ambacho kimelenga kuleta mapinduzi ya soko la Mwani kwa Ukanda wa Afrika Mashariki,
iv. Kuimarisha eneo la Mtaa wa Viwanda liliopo Dunga Zuze hii imepelekea Serikali kupokea maombi saba (7) ya Wawekezaji wa miradi ya Viwanda kutoka ndani na nje ya nchi kwa ajili wa uwekezaji wa eneo hilo,
v. Kuanza upimaji wa mafuta ya nishati yanayoingizwa nchini ambayo ni Petroli, Diseli na Mafuta ya Ndege.

105. **Mheshimiwa Spika,** Zanzibar imepiga hatua kadhaa katika uzalishaji wa maji viwandani kupitia sekta binafsi ambapo jumla ya viwanda 6; Unguja vinne ikiwemo Sky Cola Company Limited (Kibele), Lootah Group Company Limited (Drop of Zanzibar kilichopo Hanyegwa Mchana), Zainab Bottlers Company Limited (Mombasa) Safari Company Limited (Amani), Pemba Amos Industries (Lulu Chamanangwe), WaterCom Company Limited (Kinyikeni).

**k) Sekta ya Kilimo**

106. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Kilimo inayojumuisha sekta ndogo za Mazao, Mifugo na Maliasili za Misitu, wanyamapori na nyuki, sekta hii ni tegemeo kubwa kwa uchumi wa Zanzibar, na inachangia wananchi kujikimu kimaisha. Kwa kipindi cha miaka Minne mafanikio yaliyopatikana katika sekta hii ni;

i. Kukamilisha Miundombinu ya Umwagiliaji Maji katika mabonde saba (7) yenye ukubwa wa hekta 1,354; ikiwemo Bonde la Kilombero (hekta 292), Cheju A' (hekta 315) na Cheju B' (hekta 301), Kibokwa (hekta 147), Kinyasini (hekta 184), Chaani (hekta 71) na Mlemele (hekta 44).

ii. Ujenzi wa maghala mawili 2 ya kuhifadhia chakula Kizimbani kwa Unguja na Dodeani kwa Pemba yenye uwezo wa kuhifadhi tani 2,500.

iii. Kuanzisha TV Kilimo inayosaidia kuwaunganisha wakulima, wataalamu na wadau wengine wa kilimo kwa lengo la kutoa elimu, taarifa na kusambaza mbinu za kisasa za kilimo ili kuendana na hali ya soko. Tayari imeshafanikiwa kurusha vipindi 45 vya mahojiano, makala mbali mbali za kilimo 105 na vipindi 7 vya moja kwa moja (mubashara).

### l) Maendeleo ya Habari, Utamaduni na MichezoHabari

**107.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha miaka minne, Serikali imefanya mageuzi makubwa katika sekta ya habari na Michezo. Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni kama yafuatayo:-

i. Kiasi cha **TZS 157.62 bilioni** zimetumika kwa Ujenzi wa viwanja vya Michezo vya Mikoa na Wilaya, ikiwemo Viwanja vya Michezo vya Maisara (Maisara Sports Complex), Kilimani, Kitope, Kitogani, Mao Tse Tung, Gombani, Kangani na Kishindeni,

ii. Ukarabati wa viwanja vya Gombani na Amani ili kuufanya uwanja kukidhi vigezo vya CAF na FIFA,

iii. Serikali imeratibu mashindano ya Kombe la Mapinduzi kwa miaka yote minne yenye lengo la kudumisha Mapinduzi matukufu ya Zanzibar,

iv. Kufanikisha kufanyika kwa Tamasha la Mazoezi ya Viungo Kitaifa ambalo hufanyika tarehe 01 Januari, ya kila mwaka, na

v. Kuandaa na kusambaza taarifa **8,123** za matukio mbalimbali yakiwemo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa kwa wananchi kupitia Vituo vya Habari vya Umma na Binafsi.

**108.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi hichi Serikali imefanikisha usajili wa vituo vipya vya utangazaji ikiwemo; Vituo vya Radio Vitano (5); (Furaha FM, Mjini FM, KMEC Radio, Firebase FM na Crown FM). Vituo vya Televisheni Vitatu (3) (KMEC TV, Mambo Cinemax na Mambo Moto) na maudhui ya Mtandaoni 24.

- **Michezo**

**109.** **Mheshimiwa Spika,** Kutokana na kuimarika kwa uwekezaji wa Viwanja vya Michezo, sekta ya michezo imeonekana inazidi kuimarika na kuteka hisia za mashabiki, hususan

kutokana na viongozi wetu kuwa ni miongoni mwa washiriki na wachezaji mahiri wa michezo. Tunafarijika kuona hamasa za viongozi kushiriki michezo mbalimbali ikiwemo;

i. **Michezo ya Basket Ball na Tenis,** Wananchi wa Zanzibar na Afrika kwa ujumla tunajivunia uwepo wa wanamichezo kindakindaki wenye uwezo mkubwa na ushawishi wa hali ya juu, akiwemo kiongozi wetu mpendwa Dkt, Hussein Ali Mwinyi na mwenza wake Mama Maryam Mwinyi wakionesha umahiri wao wakiwa uwanjani,

ii. **Michezo ya Ngumi,** Kwa upande wa Michezo Waheshimiwa Manaibu Waziri wametoa burudani kabambe kwa kuzichapa ngumi mubashara katika uzinduzi wa viwanja vya New Amani Complex,

iii. **Mchezo wa Sky Diver,** Tumeona hamasa kubwa iliyooneshwa na Waziri wa Utalii Mheshimiwa Mudrik Ramadhan Soraga kwa kushiriki katika michezo ya Sky Dive katika kuhamasisha na kutangaza utalii nchini,

iv. **Mashindano ya Mpira wa Miguu,** Kwa mara ya kwanza SMZ imeandaa mashindano ya Kombe la Mapinduzi Cup kimataifa , ambapo fainali ya kombe hilo ilichezwa kisiwani Pemba kati ya Zanzibar Hero na timu ya Burkina Faso. Zanzibar tuliibuka na ushindi na kulitwaa kombe hilo.

v. Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi nao hawakuwa nyuma katika kuonyesha ujuzi na vipaji vya michezo ya mpira wa miguu na mikono.

**110. Mheshimiwa Spika,** Sekta hii imetanuka na kukuza pato la taifa na utalii wa Zanzibar, kwa mara ya kwanza fainali za Kombe la Shirikisho la Vilabu Barani Afrika limefanyika Zanzibar katika uwanja wa New Amaan Complex. Kupitia mchezo huu nchi yetu imezidi kujitangaza kimataifa ambapo wageni na mashabiki kutoka mataifa mengine walikuja

Zanzibar na wengine kufuatilia mubashara kwenye nchi zao. Hii inamaanisha si kukua tu kwa michezo bali imechangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi na utalii.

- **Maendeleo ya Utamaduni na Sanaa**

**111. Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanikiwa kufanya Tamasha la Utamaduni wa Mzanzibari kwa lengo la kurithisha mila, silka, desturi na tamaduni za Mzanzibari. Shughuli mbali mbali zenye mnasaba na Tamasha hilo zilifanyika zikiwemo maonyesho ya bidhaa za kitamaduni na madawa ya asili, sanaa za ngoma za asili na paredi ya wasanii na wajasiriamali iliyosheheni vionjo vya kitamaduni.

**112. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Baraza la Kiswahili imefanikiwa kuandaa Kongamano la Kiswahili la Kimataifa kila mwaka ambalo hushirikisha takriban watu 12,000 kutoka nchi mbali mbali duniani kama vile Canada, Marekani, China, Jamhuri ya Demokrasia ya Congo, Uganda, Kenya, Comoro, na wenyeji wa Tanzania Bara na Zanzibar.

**113. Mheshimiwa Spika,** Mafunzo ya ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni kwa washiriki 208 (wanaume 137 na wanawake 71) kutoka Taasisi mbali mbali za elimu yametolewa. Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wa mbinu za ufundishaji wa Kiswahili ili waweze kuzifikia na kuzitumia fursa za kukibidhaisha Kiswahili kwa kusomesha wageni ndani na nje ya nchi.

**114. Mheshimiwa Spika,** Katika kufikisha ujumbe kupitia sanaa na burudani, viongozi na wananchi kwa ujumla wanajitahidi kufikisha ujumbe katika matukio mbalimbali yakiwemo;

i. **Usomaji Utenzi,** Tumeshuhudia Waziri wetu wa Habari alivyokuwa akihamasisha lugha ya Kiswahili

kwa kutoa burudani ya mashairi nchini CUBA,

ii. **Utangazaji,** Katika ufikishaji wa taarifa za kiuchumi kwa wananchi, kupitia sanaa ya utangazaji Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Dkt. Saada Mkuya Salum alionekana akitupa habari za kiuchumi kupitia kipindi cha Taarifa ya Habari cha ZBC kinachoruka hewani kila siku.

iii. **Sanaa za Maagizo,** Kupitia msanii wetu maarufu Kirobo tunaendelea kupata elimu na burudani katika masuala mbalimbali ya maendeleo ya kiuchumi.

- **Vijana**

**115. Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana kupitia sekta hii ni kukamilika na kuzinduliwa kwa Sera ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2024, ambayo ni muongozo wa utekelezaji wa shughuli zinazohusiana na vijana.

**116. Mheshimiwa Spika,** Katika maandalizi ya bajeti hii, kwa mara ya kwanza vijana walipata fursa ya moja kwa moja kushiriki katika kutoa maoni na ushauri juu ya vipaumbele vya matumizi ya Serikali. Jukwaa hili lilikuja na ujumbe wa Kaulimbiu ***Nguvu ya Vijana kwa Uchumi imara na Maendeleo endelevu.*** Vijana **531,968** (Unguja 312,018 na Pemba 219,950) wakiwemo wanawake 286,642 na wanaume 245,326 wamefaidika kupatiwa mafunzo mbali mbali yakiwemo; Stadi za Maisha, Ujasiriamali, Stadi za Kazi, Afya ya Uzazi, Uongozi na Uzalendo, Ushiriki na Ushirikishwaji, Mabadiliko ya Tabia Nchi, Amani na Usalama na mafunzo ya TEHAMA.

### m) Maendeleo ya Jamii

**117. Mheshimiwa Spika,** Serikali kwa kuzingatia usawa wa kijinsia, wazee na watoto inaendelea kuimarisha huduma kupitia mahitaji ya msingi kwa mujibu wa makundi na haja

za jamii, maeneo ambayo yameimarishwa ni pamoja na;

i. Malipo ya Pencheni Jamii kutoka wazee 29,182 kwa malipo ya **TZS 7.0 bilioni** mwaka 2020/2021 hadi kufikia wazee 31,256 kwa malipo ya **TZS 14.42 bilioni hadi** Mwezi Aprili,2025, na

ii. Kutolewa kwa vitambulisho 31,271 (Unguja 23,190 na Pemba 8,031)vya huduma za kijamii kwa wazee wenye umri wa miaka 70, ili waweze kupatiwa huduma za kijamii, ikiwemo huduma za usafiri, matibabu na msaada kutoka kwa wadau wanaoguswa na huduma za kiustawi.

### n) Uwajibikaji na Utawala Bora

**118. Mheshimiwa Spika,** Katika kukabiliana na vitendo vya rushwa, Serikali imeimarisha Ofisi ya ZAECA kwa kufanya mabadiliko ya kisheria na kimuundo, hali iliyopelekea kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kufanikiwa kuokoa fedha za Serikali kiasi cha **TZS 4.181 bilioni**. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni;-

i. Kuimarisha matumizi ya Mifumo ya Kielektroniki ya utoaji wa huduma za utumishi wa umma, miongoni mwao ni Mfumo wa Maombi ya Ajira (Zan-Ajira), Mfumo wa Masjala ya Kielektroniki (e- Office) na Mfumo wa Taarifa za Watumishi na Malipo (Human Resource and Payroll Management Information System - HR-PayMIS).

ii. Kufanya ukaguzi kwa njia za kisasa kwa kuzingatia vipaumbele vya Serikali na kuongezeka kwa uwazi juu ya matokeo ya ukaguzi wa hesabu za Serikali kwa kuanza utaratibu wa Ripoti za Mkaguzi kuwasilishwa kwa uwazi.

**o) Masuala ya Muungano**

119. **Mheshimiwa Spika,** Serikali zote mbili zimekuwa zikifanya vikao vya mara kwa mara katika ngazi za kisekta na kitaifa ili kujadili na kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazojitokeza katika masuala ya Muungano, ambapo kwa kiasi kikubwa vikao hivyo vimesaidia kubadilishana uzoefu, utaalamu na kutatua changamoto zinazotukabili. Kwa upande wa Zanzibar kulifanyika kikao katika eneo la Nyamanzi na kuhudhuriwa na viongozi wakuu wa Serikali kilichoendeshwa na Waziri Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu wa Baraza la Wawakilishi Mheshimiwa Hamza Hassan Juma.

**p) Uimarishaji wa Wazanzibari wanaoshi Nje ya Nchi**

120. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Diaspora Serikali imeshiriki Kongamano la Wanadiaspora wa Afrika (Diaspora Africa Conference) lililofanyika Zanzibar. Kongamano hilo liliwakutanisha Wanadiaspora 100 wenye asili ya Afrika kutoka Mataifa mbali mbali Duniani ikiwemo Nigeria, Marekani, Uingereza, Urusi, Kenya na Tanzania, ambao ni wawekezaji na wafanyabiashara wakubwa.

121. **Mheshimiwa Spika,** Mageuzi makubwa yamefanyika ya kuanzisha Mfumo wa Usajili wa Diaspora wa Zanzibar, ambapo Diaspora wanaoishi nje ya nchi kupata Kadi Maalum (Diaspora Card) inayowawezesha kupata fursa kikamilifu ya kushiriki katika Maendeleo ya Zanzibar. Diaspora 800 wameshasajiliwa na 356 wamepatiwa vitambulisho, kupitia kadi hii, wanapata fursa nyingi zenye thamani kubwa, zikiwemo:-

i. Msamaha wa ada ya kibali cha kazi kwa Diaspora wanaorudi kufanya kazi nyumbani,
ii. Uwezeshaji wa kupata vibali vya ukaazi kwa urahisi,
iii. Fursa ya kufungua akaunti kwenye Taasisi za kifedha za ndani,

iv. Ukodishaji wa ardhi kwa tozo maalum, kwa ajili ya uwekezaji au matumizi binafsi,
v. Uwekezaji wa moja kwa moja kupitia ZIPA kwa gharama nafuu kutoka **USD 2,500,000** hadi **USD 200,000**,
vi. Uwekezaji katika sekta ya utalii, hata katika maeneo ambayo kwa kawaida hayaruhusiwi kwa wageni,
vii. Unafuu ya gharama za usafiri kwa boti na ndege, sawa na zile wanazolipa wananchi wa kawaida,
viii. Msamaha wa kodi katika uingizaji wa vifaa vya misaada ya kijamii kutoka nje, na
ix. Fursa ya kujitolea, kubadilishana ujuzi, utaalamu na uzoefu walioupata nje, kupitia Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali.

**122.** **Mheshimiwa Spika,** Mageuzi haya ni ushahidi wa dhamira ya kweli ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutambua, kuimarisha na kuendeleza mchango wa Diaspora katika kujenga taifa imara na lenye maendeleo jumuishi. Kwa mwaka huu wa fedha Diaspora wamepata fursa ya ushiriki wa kutoa maoni katika Majukwaa ya Bajeti na Uchumi wakati wa Maandalizi ya Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2025/2026 na maoni ya Rasimu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050.

**123.** **Mheshimiwa Spika,** Maeneo mengine ambayo Serikali inaendelea kufaidika na Diaspora Katika Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii kama yafuatayo;

i. Serikali imeratibu uingizwaji wa kontena la sadaka lililotolewa na Jumuiya ya Diaspora Ifraj Zanzibar Foundation iliyopo Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE),

ii. Kupokea Misaada kutoka Jumuiya ya Watanzania wanaoishi nchini Oman (TADIO) kwa kushirikiana na Al Wadood Charitable Group pamoja na Taasisi ya Diaspora Charity Organization ya nchini Oman,

iii. Ugawaji wa futari kwa familia 790 katika vijiji vya Mchanga wa Kwale, Kitongoji-Vunjamembe na Chonyi-Kiungoni, utoaji wa misaada ya kifedha kwa familia zenye uhitaji na ujenzi wa makaazi ya mayatima na watu wasiojiweza katika kijiji cha Mikinduni.

**124. Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanikiwa kuanzisha na kusimamia mifumo kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali, kusanifu mifumo ya TEHAMA 14 ili kuweza kurahisisha utoaji wa huduma katika Taasisi za Umma kwa haraka na ufanisi.

**q) Ulinzi na Usalama**

**125. Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kuchukua juhudi kadhaa kuhakikisha Usalama wa Raia na Mali zao unaendelea kuimarika. Kwa sasa nathubutu kusema **Nchi yetu iko salama**. Miongoni mwa hatua ambazo zinaendelea kuchukuliwa na Serikali ni pamoja na:-

i. Kuendelea kuwapa Mafunzo Maafisa na Wapiganaji lengo ni kuwajengea uwezo wa uadilifu wa kazi zao na matumizi ya mbinu bora za kushughulikia migogoro ya kiusalama na ulinzi,

ii. Kuimarisha Ulinzi wa Mipaka ya Bahari ya Zanzibar, kwa kuendesha mafunzo maalum ya operesheni za kijeshi baharini, sambamba na kutumia mfumo wa kufuatilia mwenendo na shughuli zote zinazofanywa na vyombo vyote vinavyoingia kwenye bahari ya Zanzibar kwa kushirikiana na Kikosi cha Wanamaji wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) pamoja na Mamlaka za Usafiri wa baharini ikiwemo ZMA.

**r) Sekta ya Fedha na Uchumi**

**126. Mheshimiwa Spika,** Uchumi na Fedha ndio msingi wa maendeleo yote nchini, kupitia sekta hii, kwa kipindi cha miaka minne maeneo ambayo yameimarika ni pamoja na;

i. Kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi kutoka asilimia **1.3** mwaka 2020 hadi kufikia asilimia **7.1** mwaka 2024,

ii. Kukua kwa Pato la Taifa kutoka thamani ya **TZS 4,209.0 bilion**i, mwaka 2020 hadi kufikia thamani ya **TZS 6,572.6 bilioni kwa Mwaka 2024**,

iii. Kukua kwa Pato la Mwananchi kutoka TZS 2.52 milioni sawa na Dola za Kimarekani 1,099 mwaka 2020 hadi kufikia kufikia **TZS 3.22 milioni** mwaka 2024 sawa na thamani ya Dola za Kimarekani USD 1,395,

iv. Kuongezeka kwa Miradi ya Uwekezaji kutoka 762 hadi 1,207 ambapo mitaji imeongezeka kutoka Dola za Kimarekani 7,582.9 milioni kwa mwaka 2020 hadi kufikia Dola za Kimarekani **13,519.5 milioni** mwishoni mwa mwaka 2024, na

v. Mapato yatokanayo na ada za Bima yaliongezeka kutoka **TZS 19 bilioni** mwaka 2021 hadi **TZS 130.74 bilioni** mwaka 2024.

- **Mfuko wa Hifadhi ya Jamii**

**127. Mheshimiwa Spika,** Uwekezaji wa Mfuko unajumuisha uwekezaji wa mabenki, hati fungani za Serikali na makampuni, hisa, uwekezaji wa majengo na mikopo. Hadi kufikia 31 Machi 2025, thamani ya uwekezaji wa Mfuko imefikia **TZS 1,164.98 bilioni** kutoka TZS 493.68 bilioni mwaka 2020. Ongezeko hilo linachangiwa na uwekezaji wa ziada uliofanywa kwenye masoko ya fedha TZS 885.72 bilioni na majengo TZS 344.80 bilioni.

- **Maendeleo ya Huduma za Benki**

**128. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha mwaka 2020 hadi 2024, faida ya benki imeongezeka kwa asilimia **80** kutoka **TZS 18.362 bilioni** hadi **TZS 92.086 bilioni**. Hii imetokana

na kuongezeka kwa mapato kwa asilimia **59** kutoka **TZS 82.907 bilioni** kwa mwaka 2020 hadi **TZS 201.368 bilioni** kwa mwaka 2024.

**129.** **Mheshimiwa Spika,** Ukuaji wa mapato ya benki umetokana na kuongezeka kwa makusanyo yatokanayo na riba na faida itokanayo na uwezeshaji kwa kufuata sharia na Mapato yatokanayo na matumizi ya huduma za kidigitali.

**130.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa mtaji rasilimali za benki ziliongezeka kwa asilimia 249 na kufikia **TZS 2,602.807 bilioni** hadi Machi 2025 kutoka rasilimali za **TZS 745.885 bilioni** zilizokuweko 2020. Amana za wateja hadi Machi 2025 zilifikia **TZS 2,083.277 bilioni** kutoka **TZS 591.562 bilioni** zilizokuwepo 2020.

- **Misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo**

**131.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa na mashirikiano ya karibu na Washirika wa Maendeleo kuiwezesha Zanzibar kunufaika moja kwa moja na fursa zipatikanazo kupitia Washirika wa Maendeleo (Misaada na Mikopo Yenye Masharti Nafuu) kwa ajili ya kugharamia miradi mbali mbali ya kimkakati.

**132.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanikisha upatikanaji wa Mkopo wenye masharti ya kibiashara **Euros 411 million**, kwa ajili ya kugharamia **Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba** na **Ujenzi wa Barabara Tatu** zenye urefu wa 103.5 km za Unguja na Pemba. Kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinazofadhiliwa na Benki ya CitiBank Europe Plc, Deutsche Bank na inayodhamini Taasisi ya Udhamini ya Uingereza ya United Kingdom Export Financing (UKEF).

133. **Mheshimiwa Spika,** Miradi iliyoidhinishwa katika kipindi cha miaka 4 ni Pamoja na ;

i. Ukuzaji wa Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z) **USD 150 million kutoka Benki ya Dunia.**

ii. Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati Zanzibar (ZESTA), **USD 148 million kutoka Benki ya Dunia.**

iii. Mradi wa Kuwajengea Uwezo Vijana Kujiajiri na Kuajirika Kupitia Uchumi wa Buluu (SEBEP) **USD 50 million** kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika.

iv. Ujenzi wa Hospitali ya Binguni **USD 163 million** na Hospital ya Mnazi Mmoja **USD 42.8 million** kutoka Jamhuri ya Watu wa Korea.

v. Mradi wa Umwagiliaji Maji **USD 18 millio**n ambao ni mkopo wa ziada kutoka Jamhuri ya Watu wa Korea.

vi. Mradi wa Ujenzi wa Mahkama **USD 30 million**, kutoka **Benki ya Dunia.**

vii. Mradi wa Elimu ZIQUEP **USD 50 million** kutoka Benki ya Dunia.

viii. Mradi wa Afya ya Mama na Mwana *Maternal and Child Health Investement Program* **USD 13 million** kutoka Benki ya Dunia.

ix. Programu ya Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania (Tanzania Food Resilience - TASFAM) **USD 20 million** kutoka Benki ya Dunia.

- **Ushiriki na Mahusiano ya Kijamii**

134. **Mheshimiwa Spika,** Uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi umeendelea kuakisi misingi bora ya utawala unaoweka mbele maslahi ya wananchi. Ushiriki wake wa karibu katika shughuli za kijamii kama vile kuwajulia hali wagonjwa, kushiriki misiba ya wananchi na kuswali katika misikiti mbalimbali pamoja na wananchi, si tu ni uthibitisho wa uongozi wa kua karibu na watu, bali pia ni ishara ya upendo na unyenyekevu wa kweli. Tabia hii ya

kuishi na watu, kuwapa faraja na kushiriki nao katika kila hali, imeendelea kumfanya Mheshimiwa Rais kuwa kipenzi cha wananchi na kielelezo cha utawala unaogusa maisha ya watu kwa vitendo.

- **Ushiriki Katika Shughuli za Kidini**

135. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuendeleza utamaduni wa kushirikiana, kusikiliza na kujenga umoja wa kitaifa, Mheshimiwa Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi amekutana na viongozi wa dini mbalimbali hapa nchini na nje ya nchi, na kushauriana mambo mbali mbali ya kuendeleza amani na utulivu. Huu ni ushahidi wa uongozi unaotambua nafasi ya dini katika kuimarisha maadili, amani na mshikamano wa kijamii na mfano wa uongozi unaojenga daraja la maelewano na kulinda misingi ya utawala bora kwa vitendo.

136. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mara ya kwanza Zanzibar tumeweka historia ya mahujaji wetu kusafiri na ndege ya moja kwa moja na Shirika la Ndege la Saudi Arabia, ambapo Mahujaji wameondoka Zanzibar kutoka Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abeid Amaan Karume hadi nchini Saudi Arabia katika miji ya Makkah na Madina moja kwa moja bila ya kusimama kituo chochote.

137. **Mheshimiwa Spika,** Hii ni sehemu ndogo ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha takriban miaka 4. Kwa sababu ya muda, haitowezekana kuyataja yote hapa lakini nina hakika Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako watayataja na mengi mengine katika michango yao kwenye hotuba hii.

## H. MATARAJIO YA MAPATO NA MATUMIZI JULAI-JUNI KWA MWAKA 2024/2025

### H.1 Mapato

138. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa mwenendo wa makusanyo, hadi kukamilika kwa mwezi wa Juni 2025, Serikali inatarajia kukusanya **TZS 4,057.24 bilioni** sawa na asilimia **78** ya makadirio ya **TZS 5,182.89 bilioni**.

01. **Mapato ya Ndani**

Mapato ya ndani yanatarajiwa kufikia **TZS 2,094.82 bilioni** sawa na asilimia 107 ya makadirio ya mwaka yanajumuisha;

- Mapato ya Kodi

139. **Mheshimiwa Spika,** Mapato ya kodi yanatarajiwa kufikia **TZS 1,603.45 bilioni**, sawa na asilimia 109 ya bajeti ya **TZS 1,467.06 bilioni**, kwa mchanganuo ufuatao:

i. Mamlaka ya Mapato Tanzania-Zanzibar (TRA) inatarajiwa kukusanya **TZS 658.00 bilioni** sawa na asilimia **110** ya mapato hayo;
ii. Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) inatarajiwa kukusanya **TZS 924.44 bilioni** sawa na asilimia **109.4**; na
iii. Kodi ya Mapato kutoka kwa wafanyakazi wa SMT inatarajiwa kufikia **TZS 21 bilioni** sawa na asilimia **100** ya lengo.

- **Mapato Yasiyokuwa ya Kodi**

140. **Mheshimiwa Spika,** Mapato yasiyokuwa ya kodi yanatarajiwa kufikia **TZS 279.37 bilioni** ikiwa ni asilimia **105** kwa mchanganuo ufuatao: -

i. Mapato ya Mawizara yanategemewa kufikia TZS 245.87 bilioni ikiwa ni asilimia **115** ya makadirio ya mwaka ya **TZS 213.85 bilioni**.

ii. Gawio la Mashirika ya Serikali linatarajiwa kufikia TZS 20 bilioni ikiwa ni asilimia **57** ya makadirio ya mwaka ya **TZS 35 bilioni**.

iii. Gawio la Benki Kuu ya Tanzania, linatarajiwa kufikia **TZS 13.5 bilioni** ikiwa ni asilimia **100** ya makadirio ya mwaka ya **TZS 13.5 bilioni**.

**02. Mapato Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo**

**141. Mheshimiwa Spika,** Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo yanatarajiwa kufikia **TZS 692.95 bilioni** sawa na asilimia 46 ya makadirio ya **TZS 1,516.52 bilioni**,

**03. Mapato Mengineyo**

**142. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa mapato mengineyo, matarajio ni kupatikana kiasi cha TZS 1,130 bilioni sawa na asilimia 66 ya makadirio ya TZS 1,712.00 bilioni, kati ya mapato hayo;

i. **TZS 180 bilioni** kutoka mkopo wa Hati Fungani sawa na asilimia **100** ya makadirio ya **TZS 180 bilioni** na

ii. Mkopo wa Serikali kwa Miradi ya Maendeleo **TZS 1,089.47 bilioni** sawa na asilimia **72** ya makadirio ya upatakanaji wa **TZS 1,532 bilioni**.

**04. Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi Zinazojitegemea (Own Source)**

**143. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa matarajio ni kukusanya **TZS 16.8 bilioni** sawa na asilimia **89** ya makadirio na Taasisi zinazojitegemea matarajio ni kukusanya **TZS 195.2 bilioni** sawa na asilimia **95** ya makadirio.

## H.2 Matumizi

**144. Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya Serikali hadi kufikia Juni 2025 yanatarajiwa kufikia **TZS 4,041.31 bilioni** sawa na asilimia 78 ya bajeti ya mwaka ya **TZS 5,182.89 bilioni** ambapo;

i. Matumizi ya kazi za kawaida yanatarajiwa kufikia **TZS 1,713.65 bilioni** (zikiwemo TZS 10.4 bilioni za Mamlaka za Serikali za Mitaa na **TZS 174.20 bilioni** kutoka Taasisi Zinazojitegemea);

ii. **TZS 2,321.26 bilioni** kwa ajili ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo sawa na asilimia 71 ya makadirio ya awali (kati ya hizo **TZS 1,250.49 bilioni** ni kutokana na fedha za ndani, **TZS 312.00 bilioni** kwa ajili ya Mfuko wa Kugharamia Madeni ya Miradi ya Maendeleo, **TZS 576.94 bilioni** ni mikopo na **TZS 181.83 bilioni** ni misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) na

iii. **TZS 6.4 bilion**i kwa matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**145. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Serikali inatarajia kuwa na bakaa ya **TZS 76.46 bilioni** kwa ajili ya matumizi ya awali ya mwaka mpya wa fedha.

**Kiambatisho Namba 2** Matarajio ya Mapato na Matumizi hadi kufikia Juni 2025.

## I. MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2025

**146. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2025, Uchumi wa Zanzibar unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.3 mwaka 2025 kutokana na sababu ambazo tayari tumeshaziwasilisha kupitia Hotuba ya **Mhe.Hemed Suleiman Abdulla Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar na Hotuba ya Mwelekeo wa Uchumi na Mpango wa Maendeleo imewasilishwa Barazani asubuhi ya leo**.

**147. Mheshimiwa Spika,** Matarajio ya ukuaji huo yanategemea na misingi ifuatayo:

i. Kuendelea kuimarika kwa usimamizi wa sera za kifedha;
ii. Kuimarika kwa upatikanaji wa nishati ya mafuta na gesi ili kuweza kupunguza gharama za bei za nishati hizo;
iii. Kuendelea kuimarika kwa miundombinu na huduma za bandari zetu ambazo zitapunguza gharama za upatikanaji wa huduma na bidhaa muhimu;
iv. Kuimarisha uwekezaji katika sekta ya viwanda na kuongeza thamani kwa usafirishaji wa bidhaa zilizochakatwa nje ya nchi;
v. Kuanza kwa miradi inayotarajiwa kuwa ni nyenzo za kuwezesha Zanzibar kukaribisha baadhi ya mechi za Mashindano ya Kombe la Africa (AFCON) 2027;
vi. Kutumia fursa za kiuchumi za mashindano ya wachezaji wa ndani wa Afrika (CHAN) zinazotarajiwa kuanza mwezi Agosti 2025 Tanzania; na
vii. Kuendelea kuwepo kwa hali ya amani, usalama, umoja na utulivu wa ndani, nchi jirani pamoja na duniani.

## J. MAPENDEKEZO YA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**148. Mheshimiwa Spika,** Serikali imekuwa ikichukuwa hatua maalum za kuweka utulivu wa mfumo wa kodi nchini kama njia moja wapo ya kuimarisha mazingira ya biashara, kushajiisha uwekezaji na ulipaji kodi kwa hiari. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Serikali itaendelea kuchukua hatua kadhaa za kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

**149. Mheshimiwa Spika,** Hatua hizo zinazopendekezwa kuchukuliwa na Serikali ni kama zifuatavyo;

- **Kuimarisha Uzalishaji wa Viwanda vya Ndani**

**J.1 Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Namba 8 ya Mwaka 2017**

**i. Kuongeza Kiwango cha Ushuru wa Bidhaa (Excise Duty) kwa Uingizaji wa Kuku na Samaki**

**150. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha uliopita 2024/25, Baraza la Wawakilishi liliridhia utozaji wa ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha **TZS 300** kwa uingizaji wa kilo moja ya kuku au samaki ili kuimarisha uzalishaji wa ndani, kuwa na ushindani wa haki katika soko pamoja na kuongeza ajira kwa wananchi walio wengi. Hata hivyo, bado kumeonekana kuna wimbi kubwa la uingiaji wa bidhaa hizo, hali ambayo imepelekea kutokuwepo kwa ushindani katika soko la ndani, kupungua kwa uzalishaji na ajira. Hivyo, inapendekezwa kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kutoka **TZS 300** hadi **TZS 1,000** kwa uingizaji wa kilo moja ya kuku au samaki ili kuimarisha uzalishaji wa kuku na samaki, kuwa na ushindani wa haki katika soko la ndani pamoja na kuongeza ajira. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa **TZS 7.25 bilioni**.

**J.2 Marekebisho ya Sheria ya Fedha Namba 9 ya Mwaka 2015**

**i. Kutoza Kodi ya Miundombinu kwa Uingizaji wa Bidhaa**

**151. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha kwamba, Serikali inavilinda na kuvikuza viwanda vya ndani pamoja na kuwa na ushindani halali wa biashara na bidhaa zinazoingizwa Zanzibar, inapendekezwa kama ifuatavyo:-

a. Kutoza Kodi ya Miundombinu kwa kiwango cha TZS 50 kwa lita moja ya maji safi na salama (bottled water) yanayoingia Zanzibar;

b. Kutoza Kodi ya Miundombinu kwa uingizaji wa trea moja ya mayai kwa kiwango cha TZS 1,000;

c. Kutoza kodi ya Miundombinu kwa uingizaji wa lita moja ya "soft drink", "carbonated juice" na "non-alcoholic beverage" kwa kiwango cha asilimia tano (5%); na

d. Kutoza kodi ya Miundombinu kwa kiwango cha asilimia moja (1%) kwa usafirishaji wa bidhaa. na

e. Kutoza kodi ya Miundombinu kwa uingizaji wa Mifuko (Non - Woven Bags) kwa kiwango cha asilimia tano (5%).

**152. Mheshimiwa Spika,** Hatua hizo zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa **TZS 2.27 bilioni** ambapo fedha zake zitatumika kuchangia mfuko wa maji kwa ajili ya kuimarisha huduma za maji;

- **Kuimarisha Udhibiti na Usimamizi wa Forodha**

**J.3 Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Namba 8 ya Mwaka 2017**

**i. Kuongeza Kiwango cha Ushuru wa Bidhaa kwa Uingizaji wa Mvinyo na Vinywaji Vikali**

**153. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/26, Serikali inapendekeza kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwa uingizaji wa vinywaji vikali kama ifuatavyo: -

a. Kutoza ushuru wa bidhaa kwa uingizaji wa vinywaji vikali (spirit) kutoka **TZS 4,386.06** hadi **TZS 6,000** kwa lita; na

b. Kutoza ushuru wa bidhaa kwa uingizaji wa mvinyo (wine) kutoka **TZS 4,386.06** hadi **TZS 6,000** kwa lita;

**154. Mheshimiwa Spika,** Hatua hizo zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa **TZS 1.25 bilioni** ambapo fedha zake zitatumika kwa ajili ya kuimarisha Mfuko wa Afya.

**ii. Kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa Uingizaji wa Ladha ya Sheesha (Sheesha Flavour)**

**155. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha uliopita 2024/25, Serikali ilitoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 120 kwa uingizaji wa "sheesha" ili kuwalinda vijana ambao ndio nguvu kazi kwa taifa. Hata hivyo, bado kumekuwa na wimbi kubwa la ongezeko na matumizi ya bidhaa hizo nchini, hali ambayo imepelekea matumizi ya bidhaa hiyo kuongezeka kwa vijana. Hivyo, inapendekezwa kutoza kiwango maalum (specific rate) cha ushuru wa bidhaa cha TZS 28,232 kwa uingizaji wa kilo moja ya ladha ya sheesha (flavoured sheesha) ili kupunguza matumizi ya bidhaa hiyo kwa vijana.

**156. Mheshimiwa Spika,** Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa **TZS 1.27 bilioni** na fedha zake zitatumika kwa ajili ya kuimarisha Mfuko wa Afya.

**iii. Kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa Uingizaji wa Peremende Biskuti na Chakileti**

**157. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka Fedha 2025/26, Serikali inapendekeza kuanza kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa Uingizaji wa Peremende, Biskuti na Chakileti nchini kwa kiwango cha TZS 1,000 kwa kilo moja ili kupunguza matumizi ya bidhaa hiyo ambayo yanaathiri afya ya wananchi wetu hususan watoto wadogo.

**158. Mheshimiwa Spika,** Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa **TZS 0.5 bilioni**. Aidha, fedha hizo zitatumika kwa ajili ya kuchangia mfuko wa Afya.

**iv. Kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa Uingizaji wa Bidhaa za Plastiki (Disposable Items)**

159. **Mheshimiwa Spika,** Kumekuwa na ongezeko kubwa la uingizaji wa bidhaa za plastiki (disposable items) zikiwemo sahani, gilasi na bakuli, ambapo huchafua mazingira kwani huchukua muda mrefu bila ya kuoza baada ya kutumika. Hivyo, inapendekezwa kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha 5% kwa kilo moja kwa uingizaji wa bidhaa hizo ili kuhifadhi mazingira.

160. **Mheshimiwa Spika,** Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa **TZS 0.547 bilioni**. Aidha, fedha hizo zitatumika kwa ajili ya kuchangia mfuko wa Mazingira.

**v. Kuweka utaratibu wa kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa uingizaji wa Gari kubwa zenye uchakavu wa zaidi ya Miaka Mitano**

161. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha mazingira pamoja na hali ya tabia nchi, inapendekezwa kuweka utaratibu wa kutoza ushuru wa bidhaa kwa uingizaji wa gari zenye miaka zaidi ya mitano (5) hadi kumi (10) tokea kutengenezwa kwake kwa kiwango kilichokuwepo sasa cha asilimia kumi na tano (15%).

162. **Mheshimiwa Spika,** Hatua hizo zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa **TZS 1.27 bilioni**. Aidha, fedha hizo zitatumika kwa ajili ya kuchangia mfuko wa Mazingira.

### J.4 Marekebisho ya Sheria ya Usafiri Baharini Zanzibar Nam. 5 ya 2006

**i. Kuweka Sharti la Kuwasilisha Cheti cha Uthibitisho wa Ulipaji Kodi (Certificate of Custom Clearance) Wakati wa Usajili wa Vyombo vya Baharini.**

**163. Mheshimiwa Spika,** Kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya vyombo vya baharini kuingia nchini na kusajiliwa bila ya kulipa kodi kwa mujibu wa Sheria husika, ambapo hupelekea upotevu wa mapato ya Serikali. Hivyo, inapendekezwa kufanya marekebisho katika Sheria ya Usafiri Baharini Zanzibar Nam. 5 ya 2006 kwa kuweka sharti la kuwasilisha cheti cha uthibitisho wa ulipaji wa kodi ( Certificate Tax Clearance) wakati wa usajili wa vyombo vya baharini.

**Kuimarisha Ufanisi katika Udhibiti wa Vyombo vya Moto**

**J.5 Marekebisho ya Sheria ya Usafiri wa Barabara Nam. 7 ya Mwaka 2003**

**i. Kuimarisha Usajili katika Vyombo vya Moto kwa Kuweka Utofauti wa Namba za Usajili**

**164. Mheshimiwa Spika,** Kutokana na kuwepo kwa utaratibu wa usajili na uwekaji wa namba za aina moja kwa vyombo vyote vya moto bila ya kuangalia uhalisia wa vyombo hivyo. Hali iliyopelekea changamoto katika udhibiti na utambuzi wa haraka kwa chombo husika. Hivyo, inapendekezwa kuweka utaratibu maalum wa usajili wa vyombo vya moto kwa kuzingatia aina ya chombo husika, kwa kuweka tofauti ya namba za usajili kwa vyombo vya maringi manne, matatu na mawili ili kudhibiti na kuvitambua kwa haraka.

**ii. Kuanza Rasmi Kusajili Vyombo vya Maringi Manne, Matatu na Mawili Vinavyotumia Nishati ya Umeme Badala ya Nishati ya Mafuta**

**165. Mheshimiwa Spika,** Kumekuwa na ongezeko kubwa la matumizi ya vyombo vya maringi mawili vinavyotumia nishati ya umeme badala ya nishati ya mafuta bila kusajiliwa. Hali hiyo, inaleta changamoto ya kutambua mmiliki halisi wa chombo husika iwapo vitapata ajali au kutumika katika

shughuli za kiuhalifu. Hivyo, inapendekezwa kuanza rasmi kuvisajili vyombo vya maringi manne, matatu na mawili vinavyotumia nishati ya umeme badala ya nishati ya mafuta pakee ili kuimarisha usimamizi, udhibiti pamoja na kuongeza mapato ya Serikali.

**166. Mheshimiwa Spika** Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa **TZS 0.75 bilioni.**

**iii. Marekebisho ya Viwango vya Leseni ya Udereva**

**167. Mheshimiwa Spika,** Kwa muda mrefu sasa, Serikali imekuwa ikitoza viwango vya ada ya leseni za udereva ambavyo vimepitwa na wakati na haviendani na hali halisi ya uchumi wa Zanzibar. Hivyo, inapendekezwa kama ifuatavyo: -

a. Kutoza kiwango cha ada ya TZS 30,000 cha leseni ya udereva kwa mwaka (1);

b. Kutoza kiwango cha ada ya TZS 45,000 cha leseni ya udereva kwa miaka miwili (2);

c. Kutoza kiwango cha ada ya TZS 60,000 cha leseni ya udereva kwa miaka mitatu (3); na

d. Kutoza kiwango cha ada ya TZS 75,000 cha leseni ya udereva kwa miaka mitano (5).

**168. Mheshimiwa Spika** Hatua hizo zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa **TZS 2.57 bilioni.**

**J.6 Marekebisho ya Sheria ya Tozo la Petroli Nam. 8 ya Mwaka 2001**

**i. Kuongeza Kiwango cha Leseni ya Barabara na Tozo la Kuendeleza Barabara.**

169. **Mheshimiwa Spika** Kwa Mwaka 2025/26, inapendekezwa kufanya marekebisho ya viwango vya tozo ya Leseni ya Barabara (road license) na Tozo la Kuendeleza Barabara (road fund) kama ifuatavyo: -

a. Kuongeza tozo ya leseni ya barabara kutoka TZS 38 hadi TZS 100 kwa uingizaji wa lita moja ya mafuta ya Dizeli na Petroli; na
b. Kuongeza tozo ya kuendeleza barabara (road fund) kutoka TZS 100 hadi TZS 200 kwa uingizaji wa lita moja ya mafuta ya Dizeli na Petroli.

170. **Mheshimiwa Spika** Hatua hizi zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa **TZS 35.75 bilioni** fedha zake zitatumika katika kuboresha Miundombinu ya Barabara.

**Kuimarisha Huduma Jumuishi za Kifedha**

**J.7 Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Namba 8 ya Mwaka 2017**

**i. Kutoa Unafuu wa Ushuru wa Bidhaa kwa Taasisi za Fedha Wakati Wanaponunua Huduma Kutoka Nje ya Nchi**

171. **Mheshimiwa Spika** Taasisi za fedha zikiwemo Benki zimekuwa zikitozwa ushuru wa bidhaa wakati wa ununuzi wa huduma kutoka nje ya nchi. Hali hiyo imepelekea kuongezeka kwa gharama za utoaji wa huduma. Hivyo, inapendekezwa kutoa unafuu wa ushuru wa bidhaa kwa taasisi za fedha wakati wanaponunua huduma kutoka nje ya nchi ili kuimarisha miundombinu ya huduma za kifedha pamoja na kuongeza wigo wa huduma jumuishi za kifedha.

**Hatua za kuimarisha usimamizi na Utawala wa kodi**

**Kuimarisha ukusanyaji wa Mapato**

**i. Kugomboa Madeni ya Walipakodi**

**172.** **Mheshimiwa Spika** Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa walipakodi kuhusu malimbikizo ya madeni ya kodi yaliyochangiwa kwa kiasi kubwa na utozaji wa adhabu (penalty) na riba (interest). Hivyo, inapendekezwa kuweka utaratibu maalumu wa kugomboa madeni ya kodi, ambapo mlipakodi atawajibika kulipa kodi stahiki (principal tax) na kusamehe malimbikizo ya adhabu na riba kwa kiwango cha asilimia 100 kwa walipakodi wenye madeni waliosajiliwa katika Mamlaka za Usimamizi wa Kodi (TRA & ZRA). Aidha, msamaha huo utatolewa kwa kipindi cha miezi sita (6) kuanzia tarehe 1 Julai hadi tarehe 31 Disemba, 2025.

**173.** **Mheshimiwa Spika,** Hatua hii inatarajiwa kuongeza Mapato ya Serikali **TZS 12.75 bilioni.**

**ii. Kuongeza kiwango cha uthaminishaji kwa uingizaji wa Bidhaa**

**174.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa sasa uthaminishaji wa bidhaa zinazoingizwa nchini (Customs Valuation) hutozwa kodi kwa wastani wa asilimia ishirini (20%) hadi asilimia hamsini (50%). Aidha, viwango hivi, vimepitwa na wakati na haviendani na hali halisi ya uchumi wa Zanzibar. Hivyo, inapendekezwa kuongeza uthaminishaji wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia ishirini na tano (25%) ya kiwango cha sasa. Miongoni mwa bidhaa zinazopendekezwa kuongezwa uthaminishaji ni nondo, saruji, misumari, taizi, vinywaji vikali, mvinyo na magari.

**175.** **Mheshimiwa Spika,** Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa **TZS 37.27 bilioni.**

iii. **Kuimarisha Ukusanyaji wa Mapato yasiyokuwa ya Kodi**

176. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/26, Serikali inapendekeza Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kusimamia na kukusanya mapato yasiyokuwa ya kodi ili kuimarisha ufasini wake. Hatua hiyo inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa **TZS 7.57 bilioni.**

**Kuimarisha Huduma ya Elimu**

i. **Kutenga Asilimia Moja ya "Corporate Social Responsibility" Kuingizwa katika Mfuko wa Elimu.**

177. **Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa vipaumbele vya Serikali ni kuimarisha sekta ya elimu nchini ili kujenga taifa lenye wasomi, ambao wataitumikia nchi yetu hapo baadae. Hivyo, inapendekezwa kutenga asilimia moja ya "Corporate Social Responsibility" na Marketing kuchangia katika mfuko wa elimu.

## K. MAPENDEKEZO YA SURA YA BAJETI MWAKA WA FEDHA 2025/2026

178. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Zanzibar ni sehemu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) tunawajibika kutekeleza Mikakati ya Kimataifa na Kikanda ambapo Kauli mbiu ya Bajeti ya Mwaka 2025/2026 ni **"Kuimarisha Mapato ya Ndani na Uwekezaji wa Kimkakati kwa Ukuaji wa Uchumi Jumuishi na Maisha Endelevu".** Yaani "Boosting Domestic Revenue and Strategic Investment for Inclusive econimic Growth and Sustainable Livelihood" kaulimbiu hii imetokana na Kauli Mbiu ya pamoja ***"Inclusive Economic Transformation through Domestic Resource Mobilization and Resilient strategic Investment for Job creation and Improved Livelihoods".***

179. **Mheshimiwa Spika,** Makadirio ya Mapato yamezingatia uwezo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani kulingana na vigezo na shabaha za Kiuchumi zilizopo sambamba na maoteo kutokana na ahadi kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kupitia Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na Mikakati ya Kitaifa.

**K.1 Makadirio ya Mapato**

180. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka 2025/2026, Mapato ya Serikali yanakadiriwa kufikia **TZS 6,982.076 bilioni** ikiwa ni ongezeko la **TZS 1,799.182 bilioni** sawa na asilimia 34.7 ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka 2024/2025 ya **TZS 5,182.894 bilioni.** Kati ya fedha hizo;-

i. **TZS 2,397.838 bilioni** zimekadiriwa kukusanywa kutoka katika mapato ya ndani.
ii. **TZS 2,780.00 bilioni** zinatokana na mkopo wa ndani na nje kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.
iii. **TZS 1,444.842 bilioni** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (mikopo ya **TZS 962.742 bilioni,** misaada **TZS 361.561 bilioni,** TZS 0.539 bilioni zinatokana na Mfuko wa Pamoja wa Washirika wa Maendeleo na TZS 120.000 bilioni ni Misaada ya Kibajeti).
iv. **TZS 21.669 bilioni** Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kutokana na vyanzo vya tozo na ada.
v. Mapato yatokanayo na Taasisi za Serikali Zinazojitegemea **TZS 337.727 bilioni.**

**K.2 Makadirio ya Matumizi**

181. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imekadiria kutumia TZS 6,982.076 bilioni zikiwemo,

01. **Matumizi ya Kazi za Kawaida, TZS 2,268.267 bilioni** sawa na asilimia 34.85 ya makadirio ya bajeti yote ambayo yanajumuisha; -

i. **TZS 953.733 bilioni** Mishahara;
ii. **TZS 590.970 bilioni** Matumizi ya kuendeshea Ofisi;
iii. **TZS 538.337 bilioni,** Matumizi ya huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali;
iv. **TZS 12.5 bilioni** Matumizi ya Serikali za Mitaa kwa Mapato ya Ndani na
v. **TZS 337.727** bilioni Matumizi kwa Taasisi Zinazojitegemea.

**02. Matumizi ya Kazi za Maendeleo, TZS 4,548.809 bilioni** zimekadiriwa kutumika kwa Kazi za Maendeleo sawa na asilimia 65.15 ya bajeti yote, zikiwemo;

i. **TZS 3,231.400 bilioni** kutoka Serikalini zinajumuisha (TZS 2,427.503 bilioni Miradi mipya ya kimkakati na inayoendelea na TZS 312.000 bilioni kwa ajili ya mfuko wa kugharamia madeni na TZS 491.897 bilioni miradi mengineyo inayoendelea).
ii. **TZS 1,308.240 bilioni** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ambapo (TZS 962.742 bilioni Mkopo, na TZS 345.498 bilioni ni Misaada).
iii. **TZS 9.169 bilioni** Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. **Kiambatisho Namba 3** Sura ya Bajeti 2025/2026.

## L. VIPAUMBELE VYA KIBAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**182. Mheshimiwa Spika,** Mafanikio ya kizazi cha kesho kwa kiasi kikubwa yanatokana na jasho na shida walizobeba wazazi wa leo wakati wa harakati za kuwatengenezea safari ya mafanikio yao. Hii ina maana kuwa, mafanikio ya kesho yanatokana na uwekezaji unaofanyika leo na mustakabali wa Taifa letu linatokana na kuwajibika kwetu kwa **Ulipaji wa Kodi kwa Serikali,** huku tukiwa na imani ya kuwa; Upatikanaji wa Mapato hayo yanatumika kuwezesha upatikanaji wa Elimu bora kutokana na Majengo na

Wataalamu, Vifaa na Mishahara ya Walimu, Ujenzi wa hospitali, barabara, Masoko na mengineyo. ***Kesho ya Mafanikio Hujengwa na Leo iliyo Imara.***

**183. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Matumizi ya Serikali yamezingatia maeneo yafuatayo:

i. Maslahi ya lazima kwa Watumishi wa Umma,
ii. Mahitaji ya matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali,
iii. Miradi ya Maendeleo yenye dhima ya Serikali inayoendelea na miradi inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo,
iv. Vipaumbele vya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi vya kitaifa, ikiwemo Miradi ya Kimkakati inayoendelea na mipya inayotarajiwa kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 katika maeneo ya Miundombinu, Utalii, Uchumi wa Buluu na Huduma za Jamii.
v. Kusimamia matumizi mazuri ya miradi iliyotekelezwa kwa lengo la kuleta tija na upatikanaji wa huduma bora na endelevu kwa wananchi wote.
vi. Kutenga bajeti maalumu kwa ajili ya kuwezesha ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa Wizara na Taasisi (ikiwemo vitendea kazi).
vii. Maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge, Wawakilishi na Madiwani kwa mwaka 2025 kwa kuzingatia Sheria na taratibu pamoja na maelekezo mahsusi yatakayotolewa na Serikali.
viii. Kusimamia hali ya amani, usalama na utulivu nchini kwa muda wote.
ix. Mahitaji ya uendeshaji wa shughuli mtambuka yakiwemo:

   a. Kuwawezesha vijana, wanawake na watu wenye mahitaji maalumu na huduma za wazee.
   b. Matumizi ya tafiti za kibunifu ambazo zinaelekeza kufanikisha utekelezaji wa mipango ya kitaifa ya muda mfupi na muda mrefu.

c. Utunzaji na uhifadhi wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi yakijumuisha mazingira ya Bahari na Misitu.
d. Matumizi ya Teknolojia katika uzalishaji na utoaji wa huduma kwa lengo la kuharakisha Ukuaji wa Uchumi.

**184.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa utaratibu wetu, leo asubuhi nimewasilisha Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2025/2026, naomba kwa muhutasari kuyaainisha maeneo hayo, Serikali imetenga TZS 3,292.224 bilioni, kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi Mipya ya kimkakati na ile inayoendelea ambapo Bajeti zao tayari tumeshapitisha katika Mafungu wakati tunapitisha bajeti za Wizara na Taasisi za Serikali yakiwemo:-

**a. Kutumia Fursa za Uchumi wa Buluu**

**185.** **Mheshimiwa Spika,** Eneo hili Serikali imetenga kiasi cha TZS 428.095 bilioni sawa na asilimia 13 kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa Sera na mikakati ya kuendeleza miundombinu ya viwanda vya usarifu wa mazao ya baharini pamoja na utalii wa bahari na visiwa. Kama ifuatavyo: -

i. **TZS 205.100 bilioni** kwa ajili ya kuendeleza Ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani;
ii. **TZS 130.000 bilioni** kwa ajili ya Ujenzi wa Bandari na Jengo la Abiria eneo la Mpigaduri;
iii. **TZS 29.995 bilioni** kwa ajili ya Ujenzi wa Bandari ya Kizimkazi na ya Uvuvi Shumba;
iv. **TZS 51.000 bilioni** kwa ajili ya Ujenzi wa viwanda vya kuchakata na kuhifadhi mazao ya bahari na
v. **TZS 12.000 bilioni** kwa ajili ya Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Utalii.

## b. Mazingira Wezeshi na Kuimarisha Miundombinu

186. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea na kasi ya kuimarisha miundombinu wezeshi ya anga na nchi kavu; maeneo yenye hoteli za kitalii sambamba na kuimarisha miundombinu ya uzalishaji, usambazaji na uunganishaji wa umeme na upatikanaji wa maji safi na salama. Kiasi cha **TZS 1,201.422 bilioni** zitatumika sawa na asilimia 36.5 kwa ajili ya kutekeleza programu na miradi ifuatayo: -

- **TZS 161.500 bilioni** Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba;
- **TZS 60.000 bilioni** Ujenzi wa jengo la abiria Terminal II AAKIA;
- **TZS 22.500 bilioni** Ujenzi wa Uwanja wa Ndege Nungwi;
- **TZS 40.000 bilioni** Ujenzi wa Apron katika kiwanja cha Ndege cha AAKIA;
- **TZS 442.065** bilioni Kuendelea na kusimamia ujenzi wa barabara kuu, za ndani na barabara zinazounganisha hoteli;
- TZS 270.000 bilioni Ujenzi wa Misingi ya Maji pamoja na matengenezo ya Maziwa katika Maeneo ya Mji;
- TZS 154.558 bilioni kwa ajili ya Ukamilishaji wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji safi na salama; na
- TZS 50.799 bilioni Uimarishaji wa miundombinu ya usambazaji na uunganishaji wa umeme.

## c. Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi

187. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha Taifa linakuwa na uchumi wa kidijitali, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya mifumo ya mawasiliano ya kidijitali na miundombinu katika maeneo tengefu ya Viwanda, Biashara na maeneo huru ya kiuchumi ili kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Kiasi cha **TZS 148.914 bilioni** sawa

na asilimia 4.5 zitatumika kutekeleza programu na miradi ifuatayo:-

- **TZS 70.051 bilioni** Kuendelea kuimarisha miundombinu ya uchumi wa kidijitali;
- **TZS 35.560 bilioni** kuweka miundombinu kwa ajili ya ujenzi wa maeneo ya kuendeleza biashara na viwanda;
- **TZS 10.804 bilioni** Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonyesho Zanzibar;
- **TZS 12.500 bilioni** Kwa ajili ya Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula na
- **TZS 20 bilioni** kwa Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula.

### d. Kukuza Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii

188. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za jamii Serikali itaendelea na uimarishaji wa miundombinu ya upatikanaji wa huduma bora za jamii ikiwemo Afya, Elimu, Makaazi na Michezo. Kiasi cha **TZS 1,260.141 bilion**i sawa na asilimia 38 zitatumika kutekeleza programu na miradi ifuatayo: -

- **TZS 24.400 bilioni** Kuanza ujenzi na ukarabati mkubwa wa hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja;
- **TZS 17.564 bilioni** Ujenzi wa Hospitali ya Binguni ambayo itakua ni Taasisi ya tiba, tafiti na kufundishia;
- **TZS 300.120 bilioni** Ujenzi wa nyumba za bei nafuu katika maeneo ya Chumbuni, Kisakasaka, Nyamanzi, Kwahani, Mfikiwa, Mkungu Malofa na Saateni;
- **TZS 389.400 bilioni** Ujenzi wa kiwanja kipya cha michezo – Fumba;
- **TZS 41.184 bilioni** Ujenzi wa viwanja vya michezo vya Wilaya na Mikoa; na

- **TZS 487.473 bilioni** Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Elimu;

**e. Kuimarisha Utawala Bora na Uhimilivu**

**189. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuimarisha ulinzi na usalama pamoja na kuimarisha upatikanaji wa haki ili kuhakikisha nchi inaendelea kubaki katika hali ya utulivu na amani sambamba na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Kiasi cha **TZS 253.649 bilioni** sawa na asilimia 8 zitatumika kutekeleza programu na miradi ifuatayo: -

- **TZS 25.750 bilioni** Kutekeleza mradi wa Kuimarisha Ulinzi na Usalama;
- **TZS 13.000 bilioni** Kukamilisha Ujenzi wa Mahakama za Wilaya na Mikoa;
- **TZS 4.5 000 bilioni** Kutekeleza miradi ya uhifadhi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi na
- **TZS 210.399 bilioni** Ulipaji wa Fidia za Miradi ya Maendeleo.

**Bajeti Inayozingatia Jinsia na Usawa kwa Mwaka 2025/2026**

**190. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka 2025/2026 Serikali imetenga kiasi cha **TZS 71.93 bilioni** sawa na ongezeko la asilimia 21 ikilinganishwa na **TZS 59.48 bilioni** iliyopangwa kutumika kwa Mwaka 2024/2025. Fedha hizi zinatarajiwa kutumika kwa wizara nane zinazojumuisha ongezeko la Wizara mbili za mfano ambazo ni Wizara ya Maji, Nishati na Madini pamoja na Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji.

**191. Mheshimiwa Spika,** Fedha zimepangwa kutumika katika maeneo mbalimbali ya kuimarisha usawa wa kijinsia ili kuweza kufikiwa malengo yaliyopangwa katika ngazi ya kitaifa. Wizara hizo kupitia Hotuba zao za Mwaka 2025/2026 walizoziwasilisha kwenye Baraza hili wameainisha maeneo hayo pamoja na shabaha walizojiwekea.

**192. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka 2025/2026 Serikali imeandaa Maeneo Makuu saba (Thematic areas) ya Jinsia na Usawa ambayo yametokana na uchambuzi wa kutokuwepo uwiano (Gender gaps) wa kijinsia yakiwemo;

i. Elimu, Ujuzi na TEHAMA,
ii. Ushirikishwaji wa Kiuchumi wenye Tija,
iii. Uongozi na Ushiriki wa kidemokrasia,
iv. Upatikanaji wa Huduma za Kijamii,
v. Udhalilishaji wa Kijinsia na Utawala Bora,
vi. Usawa wa Kijinsia na Uhifadhi wa Mazingira, na
vii. Usawa katika Uchumi Mkuu na Usimamizi wa Fedha za Umma.

## N. UGHARAMIAJI WA NAKISI YA BAJETI

**193. Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kutekeleza sera za kibajeti ambazo zinaiwezesha ukuaji wa Mapato ya ndani kwa kufanya mageuzi katika njia za ukusanyaji sambamba na kufanya mapitio ya Sera na Sheria ili kuhakikisha ukusanyaji wa kodi na tozo mbali mbali zinaongezeka kupitia matumizi sahihi ya mifumo ya kielektroniki na ukuaji wa uchumi kupitia utekelezaji wa miradi ya kimkakati. Kwa Mwaka 2025/2026, Serikali inatarajia kukopa TZS 2,780.00 bilioni ikiwa ni mikopo ya Hati Fungani na mikopo ya Kibiashara kupitia Taasisi za kifedha, kwa ajili ya kuziba nakisi ya Bajeti, kwa lengo la kugharamia utekelezaji wa miradi ya kimkakati.

## O. HALI YA UTEGEMEZI KWA MWAKA 2025/2026

**194. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kiwango cha utegemezi wa Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kimepungua kutoka asilimia 6.3 iliyoripotiwa mwaka jana hadi kufikia asilimia 4.9 kwa mwaka huu wa Fedha 2025/2026. Kupungua huku kunatokana na mkakati wa Serikali wa kuimarisha ukusanyaji wa Mapato

katika vyanzo vyengine na hivyo mchango tunaotarajia kupokea unatokana na Misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo wa **TZS 345.498 bilioni** umeshuka ukilinganisha na makadirio ya matumizi ya **TZS 6,982.076 bilioni.**

## P. MAZINGATIO YA MAENEO MAHSUSI KWA BAJETI YA 2025/2026

**195. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Serikali imepanga kufanya Mageuzi mbalimbali ya kisera katika maeneo ambayo yataimarisha ukusanyaji wa Mapato na kuimarisha hali ya kiuchumi Zanzibar. Miongoni mwa maeneo ambayo yatatekelezwa ni pamoja na;-

i. Kuanzisha na kuendeleza mifuko ya fedha kwa ajili ya kuimarisha Huduma za Kijamii ikiwemo; Mfuko wa Huduma ya Sekta ya Afya kwa kuiongezea vyanzo vipya vya fedha, Mfuko wa Maendeleo ya Elimu, Mfuko wa Maendeleo ya Maji na Mfuko wa Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira,

ii. Kufanya mageuzi kwa Taasisi zinazosimamia Ukusanyaji wa Mapato kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya Wizara kwa kumpa usimamizi huo Mamlaka ya Mapato Zanzibar,

iii. Kuanzisha Taasisi ya Uchumi Halali hapa Zanzibar (Zanzibar Halal Bureau) ambayo itasimamia kuthibitisha uhalali wa shughuli zote za utoaji wa huduma na bidhaa kwa wageni na wenyeji, ambayo itawezesha Serikali kuongeza soko la Utalii halali hususan kutoka ukanda wa Mashariki ya Kati,

iv. Kufanya mapitio na marekebisho katika Sheria za kodi na misamaha ili kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa Mapato ya Serikali,

v. Kuweka Mkakati maalum wa matumizi ya Mifumo ya Kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato kwenye Wizara na Taasisi za Serikali,

vi. Kuandaa mazingira rafiki kwa wananchi na wafanyabiashara kutumia mifumo ya kielektroniki wakati wanapofanya malipo bila ya kutumia fedha taslimu (cashless economy),
vii. Kusimamia uendeshaji wa shughuli za Uchaguzi Mkuu wa Serikali,
viii. Kuanza utekelezaji wa Soko la Mitaji la Zanzibar (Zanzibar Securities Exchange),
ix. Kuweka Mkakati mahsusi katika uwekezaji wa sekta ya kilimo kupitia Green House na uimarishaji wa zao la karafuu,
x. Kuimarisha maendeleo ya mtoto na makuzi wakati anapopata elimu, kwa kuchukuwa hatua za kupunguza matumizi na vinywaji vinavyoengeza kasi maradhi yasiyoambukiza (Non comunicable Deseases) hususani kwa watoto,
xi. Kutenga fedha kwa ajili ya matumizi ya dharura ya kiasi cha **TZS 100 bilioni** ikiwemo maafa ya kimaumbile,
xii. Kutengwa bajeti maalumu ya kiasi cha **TZS 373.44 milioni** kwa ajili ya ruzuku ya uendeshaji wa huduma za mabaraza ya wazee,
xiii. Kiasi cha **TZS 2.554 bilioni** zimetengwa kwa ajili ya malipo ya maposho maalum kwa walimu wakuu na wasaidizi wao,
xiv. Kutenga fedha kwa ajili ya malipo ya maposho maalum kwa Makatibu wa Wakuu wa Mikoa,
xv. Kwa Mwaka 2025/2026, Serikali imetenga kiasi cha **TZS 3.2 bilioni** kwa ajili ya ongezeko la Mishahara kwa Waheshimiwa Madiwani na Masheha.

**196. Mheshimiwa Spika,** Leo tarehe 12 Mwezi wa Juni Mwaka 2025; Baraza hili linakamilisha muhula wa mwanzo wa Serikali ya awamu ya nane (8) inayoongozwa na Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Naomba kutumia nafasi hii kwa uchache kuzungumzia hali inayoikabili nchi yetu. Kwa mujibu wa utaratibu wetu wa kidemokrasia, kila baada ya miaka

mitano nchi yetu inafanya Uchaguzi, kuchagua Viongozi wa kusimamia Maendeleo yetu katika miaka mitano inayofuata kupitia Uchaguzi Mkuu.

**197. Mheshimiwa Spika,** Suala la Amani ni Tunu ya Tanzania, Mageuzi haya tunayoyashuhudia ya kiuchumi na kijamii ni matokeo ya amani tuliyonayo. Nichukue fursa hii kuwasihi Viongozi na Wananchi wenzangu juu ya matumizi ya Kalamu, Midomo na ndimi zetu, hatukatazwi kuzungumza kwani ni moja kati ya haki ya msingi kwa kila mwanaadamu, bali tunapaswa kuchukua tahadhari juu ya athari ya matumizi ya kufikisha ujumbe. Tusitawaliwe na kusukumwa na hisia na jazba hazitotufikisha mahala pazuri kama ni maendeleo Alhamdulillah ***bila ya shaka kodi zetu tunaziona, na zinaakisi na kauli ya Uongozi Unaoacha alama,*** kinachofuata ***Yajayo Ni Neema zaidi.***

**198. Mheshimiwa Spika,** Nyota na mwanga wa kiongozi wetu Dkt. Hussein Ali Mwinyi ilianza kubainishwa na marehemu Dkt, John Pombe Magufuli Rais wa Awamu ya Tano, katika mkutano wa kumtambulisha mgombea wa CCM Naomba kunukuu **"Kama atachaguliwa Mwinyi utayaona matokeo"** matokeo yake tumeyaona leo.

**199. Mheshimiwa Spika,** Haikuchukua muda tangu kuanza kwa uongozi wa awamu ya nane, gwiji na muasisi wa siasa za upinzani enzi za uhai wake Marehemu Seif Shariff Hamadi aliiona nyota hii angavu. Kwa busara aliwasihi wanachama wake naomba kunukuuu **"Kwanini tusimpe nafasi Rais wetu, tumpe nafasi na sisi tutakuwa pamoja nae na tumeona nyota njema huonekana alfajiri"** yapaswa tumuenzi kwa kuifanyia kazi kauli yake kwa vitendo.

**200. Mheshimiwa Spika,** Naomba nifikishe Ujumbe kwa wanachama wa vyama vyote vya siasa, kama nia na dhamira zetu za kweli ni kuwaletea Maendeleo wananchi

wetu, wakati umefika kwa wazanzibari sote kuwa na kauli na msimamo mmoja juu ya maendeleo ya Zanzibar kwanza. Na kwa hili, niwasihi tuungane na Chama cha Mapinduzi, kwa lengo la kuendeleza mageuzi ya kiuchumi ya Zanzibar, njia iko safi na matendo yanaonekana.

## Q. SHUKURANI

**201.** **Mheshimiwa Spika,** Napenda kumalizia Hotuba yangu kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuendelea kuipambania Zanzibar kwa hali zote. Baraka hii kubwa ambayo nchi yetu imeipata si jambo la bahati tu, bali ni matokeo ya maombi ya dhati yaliyofanyika katika Misikiti yote ya Unguja na Pemba. Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amekuwa akienda kuswali na kuungana na waumini katika kila Mkoa, Wilaya, Vijiji na Mitaa mbali mbali jambo linalochangia kuimarika kwa mshikamano, amani na ustawi wa jamii.

**202.** **Mheshimiwa Spika,** Uongozi wake thabiti, maono makubwa na dhamira ya dhati ya kuwaletea wananchi maendeleo ya kweli. Kupitia maelekezo yake na msukumo wake katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati, Serikali imeweza kuimarisha uchumi, kukuza huduma za kijamii na kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma. Kwa hahika Wananchi wanaziona Kodi zao na wanatambua na kuthamini juhudi zake za kukuza uchumi

**203.** **Mheshimiwa Spika,** Kipekee nitoe shukurani zangu za dhati kwako wewe binafsi. Spika wa Baraza la Wawakilishi ukiwa kiongozi wa muhimili wa Baraza la kutunga Sheria (BLW), **ambalo ni nguzo adhimu kwa mustakabali wa nchi yetu,** Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid na Wasaidizi wako wote wakiwemo; Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti

wa Baraza la Wawakilishi, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu pamoja na Wajumbe wote wa Baraza hili, kwa kazi kubwa ya kuliendesha kwa umahiri mkubwa Baraza hili kwa miaka mitano hii inayomalizika na katika kikao hiki cha bajeti. Hakika mnatusaidia sana Serikali, kuweza kufikia matarajio ya wananchi wetu ya kuwaletea maendeleo na kuboresha hali zao za maisha na ustawi wao kiujumla. ***Mmetuvusha salama kwa mashirikiano na maelewano makubwa na mihimili mingine ya Serikali.***

**204.** **Mheshimiwa Spika,** Natoa shukurani makhsusi kwa Kamati nilizofanyakazi nazo kwa karibu zaidi. Ikiwemo, kamati ya Bajeti, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma na Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Mashirika (PAC) chini ya uongozi imara wa **Mheshimiwa Juma Ali Khatib** na Kamati ya Kanuni iliyoongozwa na Mheshimiwa Mihayo Juma Suleiman.

**205.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaongozwa kupitia Mihimili mitatu ukiwemo Muhimili wa Mahakama, ambao unajitegemea katika usimamizi wake, unaongozwa kwa ustadi mkubwa na **Mheshimiwa Khamis Ramadhan Abdalla** Jaji Mkuu wa Zanzibar, katika kusimamia upatikanaji wa haki kwa watu wote, kwa mujibu wa Sheria zetu. Kimsingi, Maelewano na utendaji kazi wa uendeshaji wa Nchi, kupitia Mihimili yote mitatu ni matokeo ya ***Nchi tuitakayo ya Zanzibar ni njema atakae na aje.***

**206.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Watendaji, nashukuru sana mchango mkubwa wa mfano wa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Said. Mashirikiano makubwa tumeyapata kutoka Wizara zote hivyo kwa fursa hii, nashukuru sana utendaji wa Makatibu Wakuu na watendaji wote wa SMZ.

**207.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa hili, sina budi kuwapongeza tena wasaidizi wa karibu wa Mheshimiwa Rais, Makamu wa

Kwanza wa Rais **Mheshimiwa Othman Masoud Othman** na Makamu wa Pili wa Rais **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah.** Hakika wanazitendea haki nafasi zao za kumsaidia vyema Mheshimiwa Rais bila kuchoka. Kwangu ni fahari na furaha isiyopimika kupata bahati ya kufanya kazi pamoja na viongozi hawa kwa mafanikio yasiyo mithilika ndani ya Nchi yetu.

**208.** **Mheshimiwa Spika,** Nitoe pongezi kwa msaidizi wangu wa karibu, Naibu Waziri Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango Mheshimiwa Juma Makungu Juma, kwa jitihada zake na kwa kweli amekuwa msaada mkubwa katika kusimamia na kuimarisha sekta ya fedha kwa ujumla wake, namuomba Mwenyezi Mungu azidi kumpa siha na ujasiri aweze kuwatumikia vyema wananchi wa Jimbo la Kijini katika miaka mitano ijayo.

**209.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha utekelezaji wa majukumu yangu nimepatiwa ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango. Kipekee naomba kumpongeza Katibu Mkuu Ofisi ya Rais- Fedha na Mipango, Dkt. Juma Malik Akil, Katibu Mtendaji Tume ya Mipango Dkt. Rahma Salim Mahfoudh, Naibu Katibu Mkuu Fedha na Mipango CPA. Aboud Hassan Mwinyi, Mhasibu Mkuu wa Serikali CPA. Hamad Saleh Hamad pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Rais- Fedha na Mipango kwa mashirikiano na mshikamano wao wa dhati katika kuwezesha Utekelezaji wa Majukumu yangu. Aidha, nawashukuru Makamishna wote, Msajili wa Hazina, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Wataalamu wote wa Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango kwa utendaji wao mahiri uliowezesha kukamilisha maandalizi ya Hotuba yangu kwa wakati.

**210.** **Mheshimiwa Spika,** Bila kuwasahau Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar CPA Said Kiondo Athumani

na Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa upande wa Zanzibar Ndg. Saleh H. Pandu. Pamoja na watumishi wao wote kwa kazi yao kubwa ya kujituma katika kuhakikisha kwamba mapato ya ndani yanakusanywa kwa ufanisi na kwa kuzingatia misingi ya Sheria na uwajibikaji. Mafanikio ya utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025 yametokana kwa kiasi kikubwa na juhudi zao thabiti zinazotokana na ushirikiano mzuri uliopo kati ya mamlaka hizi na wafanyabiashara pamoja na walipa kodi, katika kujenga mazingira wezeshi ya ulipaji kodi kwa hiari.

211. **Mheshimiwa Spika,** Napenda pia kutumia fursa hii kuvishukuru vyama vyote vya siasa kwa mchango wao muhimu katika kujenga mazingira ya demokrasia, amani, mshikamano na maendeleo. Kwa pamoja, tunalo jukumu la kuendeleza taifa letu kwa misingi ya haki, usawa, na uwajibikaji katika kuhakikisha kuwa maendeleo ya nchi yetu yanapatikana kwa njia shirikishi na endelevu. Tunathamini sana ushirikiano wao, ambao umewezesha mjadala wa bajeti za Wizara kuendeshwa kwa njia ya staha na yenye tija.

212. **Mheshimiwa Spika,** Naomba pia kuwashukuru Bodi na Menejimenti za Taasisi za kifedha ikiwemo Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC) na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF). Aidha, natoa pongezi kwa benki za biashara zinazofanya kazi hapa Zanzibar ikiwemo CRDB, NMB, NBC, Absa, TCB, KCB, Azania, Equity, Stanbic, Diamond Trust Bank, Exim Bank, Tanzania Agricutural Development Bank, pamoja na taasisi nyengine za kifedha kwa mchango wao mkubwa katika kuimarisha sekta ya fedha nchini. Serikali inatambua na kuthamini ushirikiano uliopo kati yake na wadau wote hao, na itaendelea kuweka mazingira mazuri ili kuziwezesha taasisi hizi kuendelea kutoa huduma zenye tija kwa wananchi wote. Tunatoa wito kwa benki na taasisi za kifedha kubuni bidhaa rafiki kwa

makundi maalumu ya kijamii na kushirikiana na Serikali katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kitaifa.

213. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Serikali, kuwashukuru wote waliochangia kufanikisha kwa namna moja ama nyengine katika uwekezaji wa Hati Fungani ya SUKUK. Aidha kuchangia, kuhamasisha au kuwezesha kupatikana kwa wawekezaji wakiwemo Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi, Wanamichezo, Diaspora,Viongozi Waandamizi na watu binafsi katika makundi yote bila kusahau kikundi cha Meli nne SACCOS, kwa uwekezaji mkubwa wa mfano waliouonyesha. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inathamini sana imani yao katika safari hii ya pamoja ya kuijenga nchi yetu kiuchumi.

214. **Mheshimiwa Spika,** Sitaitendea haki familia yangu kama sitowashukuru nao pia, kwa namna wanavyonivumilia nikiwa katika hekaheka za ujenzi imara na Uchumi Endelevu wa Taifa hili, wamenivumilia muda wote ninapokuwa mbali nao, si rahisi kwao hata kidogo kama familia wanatamani sana kuwa nami muda mwingi. Nawashukuru sana kwa maombi yao ya kunitakia kheri.

215. **Mheshimiwa Spika,** Kwa heshima na taadhima naomba nikishukuru chama changu Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kuendelea kunipa moyo na kunitia ujasiri katika utekelezaji wa majukumu ya kitaifa kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi nikiwa kama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango niwaahidi kuwa nitapambana hadi tone la mwisho kuiakisi falsafa ya Chama.

216. **Mheshimiwa Spika,** Tusisahau wala tusipuuze kazi kubwa na ya kipekee inayofanywa na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. Katika kipindi hichi, tumeshuhudia mageuzi makubwa katika sekta ya Ulinzi na Usalama, ambapo Vikosi vyetu vya SMZ vimeendelea kuonesha uwezo mkubwa si tu

katika kulinda amani, bali pia katika kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za maendeleo na uzalishaji. Leo hii, Vikosi vyetu ni sehemu ya mnyororo wa uzalishaji na ujenzi wa miradi mbali mbali kama vile Skuli, Masoko na Miundombinu mengine ya kijamii. Nawashukuru kwa dhati sana Makamanda, Maafisa, Askari na Wapiginaji wote kwa uzalendo wao, ujasiri usiotetereka na mchango wao mkubwa katika kulijenga Taifa letu. Tunawathamini, tunawaenzi na tunajivunia sana kuwa na mashujaa wa aina yao.

217. **Mheshimiwa Spika,** Kipekee nizishukuru nchi marafiki, Washirika wa Maendeleo, Mashirika ya Kimataifa, Jumuiya za Kikanda, Taasisi za Kiserikali pamoja na wadau wengine wakiwemo Sekta Binafsi kwa ushirikiano wao katika kuchangia bajeti hii inayoendelea na walioahidi kuchangia Bajeti ya Mwaka 2025/2026 zikiwemo; Austria, Germany, Korea Kusini, Oman, Netherlands na Spain. Aidha, Taasisi na Mashirika ya Kimataifa ni pamoja na; AfDB, BADEA, World Bank, UNICEF, STBF, KFW, Exim Bank, Mfuko wa Khalifa, UN-Women, USAID, EU, IFAD, UNDP, UNFPA, Global Fund, WHO, Nutrition International, JICA, UNIDO, Irish Embassy, NORAD, UNAIDS, IFAD/OPEC, ENABEL, GEF/WWF.

## R. HITIMISHO

218. **Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe Makadirio ya Mapato ya Serikali ya kukusanya **TZS 6,982.076 bilioni** (Shilingi Trilioni Sita, Bilioni Mia Tisa Themanini na Mbili, Milioni sabini na sita). Kati ya mapato hayo, **TZS 6,622.680 bilioni** Makusanyo ya Serikali Kuu. Kwa upande wa Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa **TZS 21.669 bilioni** na Taasisi za Serikali zinazojitegemea ni **TZS 337.727 bilioni,** naliomba Baraza lako tukufu kuridhia makusanyo hayo kupitia Mamlaka zao.

**219. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe **TZS 6,982.076 bilioni** (Shilingi Trilioni Sita, Bilioni Mia Tisa Themanini na Mbili, Milioni Sabini na Sita), kati ya hizo **TZS 2,433.267 bilioni** kwa ajili ya kazi za kawaida, (zinajumuisha TZS12.50 bilioni za Mamlaka za Serikali za Mitaa na TZS 337.727 bilioni za Taasisi za Serikali zinazojitegemea) na **TZS 4,548.809 bilioni** zimeelekezwa kwenye kutekeleza Mpango wa Maendeleo (zinajumuisha **TZS 9.169 bilioni** za Mamlaka za Serikali za Mitaa).

**220. Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha.

**DKT. SAADA MKUYA SALUM,**
**WAZIRI WA NCHI-OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO,**
**ZANZIBAR**
**JUNI, 2025**

## S. VIAMBATISHO

Kiambatisho Namba 1: Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha miezi tisa Julai 2024 – Machi 2025;

Kiambatisho Namba 2: Matarajio ya Mapato na Matumizi Hadi Juni 2025

Kiambatisho Namba 3: Sura ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

Kiambatisho Namba 4: Mfumo wa Bajeti kwa kipindi cha kati cha Matumizi Mwaka wa Fedha 2025/2026-2027/2028.

+

| Kiambatisho Namba: 1 UTEKELEZAJI WA BAJETI KIPINDI CHA JULAI2024-MACHI 2025 | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Halisi Julai - Machi, 2024 | Bajeti 2024/ | Makadirio Julai - Machi, 2025 | Halisi Julai - Machi, 2025 | % Bajeti | % Julai-Machi |
| **MAPATO** | | | | | | |
| | | | | | | |
| ***Mapato ya Ndani*** | ***1,085.06*** | ***1,954.37*** | ***1,494.57*** | ***1,432.34*** | ***73.29*** | ***95.84*** |
| Mapato ya Kodi - ZRA | 559.34 | 845.98 | 657.94 | 655.53 | 77.49 | 99.63 |
| Mapato ya Kodi - TRA | 373.17 | 600.08 | 442.96 | 471.04 | 78.50 | 106.34 |
| Mapato yasiyokuwa ya Kodi | 127.63 | 252.26 | 200.40 | 136.65 | 54.17 | 68.19 |
| Mapato-Wafanyakazi SMT (PAYE) | 15.75 | 21 | 15.75 | 15.75 | 75.00 | 100.00 |
| Gawio kutoka BoT | | 13.50 | 13.50 | 13.50 | 100.00 | 100.00 |
| ***Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mit*** | 9.17 | 18.94 | 13.08 | 10.33 | 54.53 | 78.97 |
| ***Mapato ya Taasisi zinazojitegemea (Transfer own source)*** | | 202.61 | 150.94 | 129.54 | 63.94 | 85.82 |
| ***Misaada na Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo*** | ***534.83*** | ***1,516.52*** | ***408.73*** | ***353.29*** | ***23.30*** | ***86.44*** |
| Misaada ya Kibajeti (GBS) | 72.97 | 100 | 82.46 | 76.58 | 76.58 | 92.87 |
| Misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 57.47 | 322.95 | 30.039 | 51.438 | 15.93 | 171.24 |
| Mfuko wa Pamoja wa Wafadhili (BF) | 0.24 | 0.26 | 0.260 | 0.272 | 104.67 | 104.67 |
| Mikopo Nafuu ya Miradi ya Kisekta | 404.15 | 1,093.31 | 295.969 | 225.274 | 20.60 | 76.11 |
| ***Mikopo ya Serikali kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo*** | ***596.63*** | ***1,712.00*** | ***353.96*** | ***418.47*** | ***24.44*** | ***118.23*** |
| Mkopo wa Serikali kwa Miradi ya Maendeleo | 487.79 | 1,532.00 | 173.96 | 135 | 8.81 | 77.60 |
| Mkopo wa Hati Fungani | 108.84 | 180.00 | 180.00 | 283.47 | 157.48 | 157.48 |
| **JUMLA YA MAPATO YA SERIKALI KUU** | **2,207.35** | **4,961.34** | **2,093.24** | **2,064.23** | **41.61** | **98.61** |
| **JUMLA YA MAPATO (Serikali Kuu + LGA +Own Source)** | **2,216.52** | **5,182.89** | **2,257.26** | **2,204.10** | **42.53** | **97.65** |
| **MATUMIZI** | | | | | | |
| **Matumizi ya Kawaida ya Serikali** | **919.76** | **1,911.79** | **1330.40** | **1208.47** | **63.21** | **90.84** |
| Mfuko Mkuu wa Huduma za Serikali | 214.96 | 436.61 | 323.86 | 284.60 | 65.18 | 87.88 |
| Mshahara Mawizara | 430.16 | 763.42 | 487.47 | 489.07 | 64.06 | 100.33 |
| Mshahara Ruzuku | 82.92 | 130.17 | 94.053 | 94.25 | 72.41 | 100.21 |
| Matumizi Mengineyo Mawizara | 131.92 | 277.76 | 190.307 | 164.70 | 59.30 | 86.54 |
| Matumizi Mengineyo Taasisi zinazopoke | 55.41 | 90.31 | 64.24 | 49.35 | 54.65 | 76.83 |
| **Matumizi ya Serikali za Mitaa kwa Mapato ya Ndani** | 4.39 | 10.91 | 10.47 | 9.84 | 90.21 | 94.00 |
| **Matumizi kwa Taasisi zinazojitegemea** | | 202.61 | 160.01 | 116.65 | 57.57 | 72.90 |
| **Matumizi ya Maendeleo** | **1299.49** | **3,271.10** | **1,118.86** | **1,174.69** | **35.91** | **104.99** |
| Fedha za Serikali | 562.85 | 1,550.00 | 627.53 | 858.40 | 55.38 | 136.79 |
| Mkopo kutoka Washirika wa Maendeleo | 404.15 | 1,093.31 | 195.97 | 117.79 | 10.77 | 60.11 |
| Misaada kutoka Washirika wa Maendele | 57.47 | 307.76 | 50.04 | 34.14 | 11.09 | 68.23 |
| Mfuko wa Kugharamia Madeni (Debt Ser | 273.44 | 312.00 | 241.12 | 162.78 | 52.17 | 67.51 |
| Matumizi ya Serikali za Mitaa | 1.58 | 8.03 | 4.20 | 1.58 | 19.64 | 37.56 |
| **JUMLA YA MATUMIZI** | **2219.25** | **5,182.89** | **2,449.26** | **2,383.16** | **45.98** | **97.30** |

**Kiambatisho Namba:2 Matarajio ya Mapato na Matumizi hadi Juni 2025**

**MATARAJIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI ( LIKELY OUTTURN) KWA MWAKA 20224/2025**

| | | | |
|---|---|---|---|
| | **Tarakimu ni TZS "Bilioni"** | | |
| **A: MAPATO** | | | |
| **MAELEZO** | **Bajeti iliyoidhinishwa 2024/2025** | **Matarajio Hadi Juni 2025** | **Asilimia** |
| **Mapato ya Ndani na Halmashauri na Taasisi zinazojitegemea** | **1,954.38** | **2,094.82** | **107%** |
| ***Mapato ya Ndani*** | ***1,732.82*** | ***1,882.82*** | **109%** |
| ZRA | 845.98 | 924.44 | 109% |
| TRA | 600.08 | 658.00 | 110% |
| Mapato yasiyokuwa ya Kodi | 265.76 | 279.37 | 105% |
| Mapato - Wafanyakazi wa SMT | 21.00 | 21.00 | 100% |
| ***Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa*** | ***18.94*** | 16.80 | 89% |
| **Mapato ya Taasisi zinazojitegemea (Transfer own source)** | ***202.61*** | 195.20 | 96% |
| ***Mapato ya Washirika wa Maendeleo*** | **1,516.52** | **692.95** | **46%** |
| Msaada wa Kibajeti (GBS) | 100.00 | 100.00 | 100% |
| Mfuko wa Pamoja wa Wafadhili (BF) | 0.26 | 0.27 | 105% |
| Misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 322.95 | 161.83 | 50% |
| Mkopo Nafuu ya Kisekta | 1,093.31 | 430.85 | 39% |
| ***Mapato Mengineyo*** | ***1,712.00*** | ***1,269.47*** | **74%** |
| Mkopo wa Ndani | 180.00 | 180.00 | 100% |
| Mkopo wa Serikali kwa Miradi ya Maendeleo | 1,532.00 | 1,089.47 | 71% |
| **Jumla Kuu** | **5,182.89** | **4,057.24** | **78%** |
| **B: MATUMIZI** | | | |
| **Matumizi ya Kawaida** | ***1,911.78*** | ***1,713.65*** | **90%** |
| Mshahara Mawizara | 763.41 | 751.56 | 98% |
| Mshahara Ruzuku | 130.17 | 131.00 | 101% |
| Matumizi Mengineyo Mawizara | 277.76 | 152.09 | 55% |
| Matumizi Mengeneyo Ruzuku | 90.31 | 69.50 | 77% |
| Mfuko Mkuu wa Serikali | 436.61 | 424.90 | 97% |
| Matumizi ya Serikali za Mitaa kwa Mapato ya Ndani | 10.91 | 10.40 | 95% |
| Matumizi ya Taasisi zinazojitegemea | 202.61 | 174.20 | 86% |
| **Matumizi ya Maendeleo** | ***3,263.08*** | ***2,321.26*** | **71%** |
| Fedha za Serikali | 1,550.00 | 1,250.49 | 81% |
| Mfuko wa Kugharamia Madeni ya Miradi ya Maendeleo (Debt Services Fund) | 312.00 | 312.00 | 100% |
| Misaada Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 307.76 | 181.83 | **59%** |
| Mkopo Nafuu ya Kisekta kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 1,093.32 | 576.94 | **53%** |
| **Jumla Ndogo** | ***5,174.86*** | ***4,034.91*** | **78%** |
| **Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka Vianzio vyao** | ***8.03*** | 6.40 | **80%** |
| **Jumla Kuu** | ***5,182.89*** | ***4,041.31*** | **78%** |

***Chanzo:*** *OR - Fedha na Mipango*

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Kiambatisho Namba :3** | | | | |
| | **SURA YA BAJETI 2025/2026** | | | | |
| | **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026** | | | | |
| | | | | **TZS Bilioni** | |
| | **MAPATO** | **2024/2025** | | **2025/2026** | |
| **A** | **Mapato ya Ndani (ikijumuisha na halmashauri na Taasisi zinazojitegemea)** | | **1,954.38** | | **2,757.235** |
| **1** | **Mapato ya Kodi na Non Tax** | | **1,732.82** | | **2,397.838** |
| | *(i) Mapato ya Kodi -ZRA* | 845.98 | | 1,257.240 | |
| | *(ii) Mapato ya Kodi - TRA* | 600.08 | | 825.770 | |
| | *(iii) Mapato yasiyokuwa ya Kodi* | 265.76 | | 293.829 | |
| | *(iv) Mapato ya Kodi za Wanyakazi kutoka SMT (PAYE)* | 21.00 | | 21.000 | |
| **2** | **Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa** | **18.94** | 18.94 | 21.669 | 21.669 |
| **3** | **Mapato ya Taasisi zinazojitegemea (Transfer own source)** | **202.61** | 202.61 | 337.727 | 337.727 |
| **B** | **Misaada na Mikopo Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo** | | **1,516.52** | | **1,444.842** |
| | *(i) Misaada ya Kibajeti (GBS)* | 100.00 | | 120.000 | |
| | *(ii) Misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo* | 322.95 | | 361.561 | |
| | *(iii) Mikopo Nafuu ya Miradi ya Kisekta* | 1,093.31 | | 962.742 | |
| | *(iv) Mfuko wa Pamoja (Basket Fund)* | 0.26 | | 0.539 | |
| **C** | **Mikopo ya Serikali kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo** | | **1,712.00** | | **2,780.000** |
| | *(i) Mikopo wa Serikali kwa Miradi ya Maendeleo* | 1,532.00 | | 1,700.000 | |
| | *(ii) Mikopo ya Hati Fungani* | 180.00 | | 1,080.000 | |
| | **Mapato ya Serikali Kuu** | | **4,961.34** | | **6,622.6800** |
| | **JUMLA YA MAPATO (A+B+C)** | | **5,182.894** | | **6,982.0761** |
| | **MATUMIZI** | | | | |
| **E** | **Matumizi Ukijumuisha (Halmashauri na Taasisi zinazojitegemea)** | | **1,911.79** | | **2,433.2667** |
| | **Matumizi ya Kawaida** | | **1,698.27** | | **2,083.040** |
| | **(i) Mfuko Mkuu wa Huduma za Serikali** | **436.6055** | | **538.337** | |
| | *Malipo ya Riba za Ndani na Mitaji* | 131.11 | | 304.640 | |
| | *Matumizi mengineyo ya Mfuko Mkuu wa Serikali* | 305.50 | | 233.697 | |
| | **(ii) Mshahara** | **893.596** | | **953.733** | |
| | *Mshahara Mawizara* | 681.18 | | 703.947 | |
| | *Mshahara Ruzuku* | 130.17 | | 142.808 | |
| | *Michango ya Serikali katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ( ZSSF)* | 62.30 | | 85.582 | |
| | *Mfuko wa Huduma ya Afya ZHSF* | 19.95 | | 21.396 | |
| | **(iii) Matumizi mengineyo** | **368.0665** | | **590.970** | |
| | *Matumizi Mengineyo Mawizara* | 277.76 | | 269.801 | |
| | *Matumizi Mengineyo ya Taasisi zinazopokea Ruzuku* | 90.31 | | 108.889 | |
| | ***Matumizi maalum kulingana na Sera za Matumizi "Protected Expenditure"*** | | | 212.280 | |
| | **(iv)Matumizi ya Serikali za Mitaa kwa Mapato ya Ndani** | **10.911** | 10.91 | 12.500 | 12.500 |
| | **(v) Matumizi kwa Taasisi zinazojitegemea( Transfer of Expenditures)** | **202.607** | 202.61 | 337.727 | 337.727 |
| **F** | **Matumizi ya Maendeleo Ukijumuisha (Halmashauri na Taasisi zinazojitegemea)** | | **3,271.11** | | **4,548.809** |
| | **Matumizi ya Miradi ya Maendeleo** | | 3,263.07 | | **4,539.640** |
| | (i) Fedha za Serikali Miradi Mipya ya Kimkakati na inayoendelea | 777.76 | | 2,427.503 | |
| | *(ii) Mkopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo* | 1,093.31 | | 962.742 | |
| | *(iii) Misaada kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo* | 307.76 | | 345.498 | |
| | *(iv) Mfuko wa Kugharamia Madeni ya Miradi ya Maendeleo (Debt Services Fund)* | 312.00 | | 312.000 | |
| | *(v) Miradi Mengineyo* | 772.25 | | 491.897 | |
| | *(vi) Matumizi ya Serikali za Mitaa* | **8.03** | 8.03 | 9.169 | 9.169 |
| | **Matumizi Serikali Kuu** | | **4,961.34** | | **6,622.680** |
| | **JUMLA MATUMIZI (E+F)** | | **5,182.89** | | **6,982.076** |
| | *Chanzo:OR- Fedha na Mipango* | | | | |

| Kiambatisho Namba :4 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MFUMO WA BAJETI KWA MWAKA 2025/2026-2027/2028** | | | | |
| | Tarakimu ni TZS "bilioni" | | | |
| **MAELEZO** | **Bajeti Iliyoidhinishwa 2024/2025** | **Makadirio 2025/2026** | **Makadirio 2026/2027** | **Makadirio 2027/2028** |
| **Mapato ya Ndani na Halmashauri** | **1,954.376** | **2,757.235** | **3,176.083** | **3,812.912** |
| **Mapato ya Ndani** | **1,732.825** | **2,397.838** | **2,748.585** | **3,302.318** |
| Mapato ya Kodi - ZRA | 845.979 | 1,257.240 | 1,398.405 | 1,674.732 |
| Mapato ya Kodi - TRA | 600.082 | 825.770 | 970.515 | 1,174.683 |
| Mapato yasiyokuwa ya Kodi (Wizara na Taasisi ) | 265.764 | 293.829 | 358.664 | 431.904 |
| Makusanyo ya Kodi za Wanyakazi kutoka SMT (PAYE) | 21.000 | 21.000 | 21.000 | 21.000 |
| ***Mapato ya Halmashauri*** | ***18.944*** | ***21.669*** | ***22.226*** | **24.268** |
| **Mapato ya Taasisi zinazojitegemea ( own source)** | ***202.607*** | ***337.727*** | ***405.272*** | ***486.327*** |
| **Mapato ya ODA** | **1,516.516** | **1,444.842** | **1,464.727** | **1,262.679** |
| Mfuko wa Pamoja wa Wafadhili (BF) | 0.260 | 0.539 | 0.560 | 0.600 |
| Ruzuku kutoka Nje | 322.947 | 361.561 | 252.039 | 319.752 |
| Mkopo kutoka Nje | 1,093.309 | 962.742 | 1,062.129 | 762.328 |
| Msaada wa Kibajeti (GBS) | 100.000 | 120.000 | 150.000 | 180.000 |
| **Mapato Mengineyo** | **1,712.000** | **2,780.000** | **3,050.000** | **3,200.000** |
| Mkopo wa Ndani /TB | 180.000 | 1,080.000 | 1,300.000 | 1,400.000 |
| Mkopo wa Serikali kwa Miradi ya Maendele | 1,532.000 | 1,700.000 | 1,750.000 | 1,800.000 |
| ***Jumla Kuu*** | **5,182.892** | **6,982.076** | **7,690.811** | **8,275.592** |
| **Matumizi ya Kawaida** | **1,911.778** | **2,433.267** | **2,795.449** | **3,245.200** |
| Mshahara Mawizara | 681.158 | 703.947 | 731.231 | 870.231 |
| Mshahara Ruzuku | 130.170 | 142.808 | 149.949 | 179.938 |
| Matumizi Mengineyo Mawizara | 277.760 | 482.081 | 515.827 | 721.112 |
| Matumizi Mengeniyo Ruzuku | 90.310 | 108.889 | 110.650 | |
| Mfuko Mkuu wa Serikali | 305.500 | 233.697 | 298.052 | 395.430 |
| Malipo ya Ribaza Ndani na Mtaji | 131.110 | 304.640 | 456.960 | 457.417 |
| Michango ya Serikali katika Mifuko ya Jamii | 62.300 | 85.582 | 92.530 | 99.530 |
| Mfuko wa Huduma ya Afya -ZHSF | 19.950 | 21.396 | 22.465 | 22.690 |
| Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Makusanyo yao ya Ndani | 10.910 | 12.500 | 12.513 | 12.525 |
| Mapato ya Taasisi zinazojitegemea ( own sou | 202.610 | 337.727 | 405.272 | 486.327 |
| **Matumizi ya Maendeleo** | **3,271.114** | **4,548.809** | **4,895.362** | **5,030.391** |
| Fedha za Serikali kwa Miradi ya Maendeleo | 1,550.000 | 2,919.400 | 3,066.742 | 3,220.079 |
| Mfuko wa Kugharamia ulipaji wa Madeni ya Miradi ya Maendeleo | 312.000 | 312.000 | 330.000 | 340.000 |
| Fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 1,401.084 | 1,308.240 | 1,486.910 | 1,457.602 |
| Matumizi ya Miradi ya Maendeleo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Makusanyo yao ya Ndani | 8.030 | 9.169 | 11.710 | 12.710 |
| **Jumla ya Matumizi** | **5,182.892** | **6,982.076** | **7,690.811** | **8,275.592** |
| ***Chanzo: Afisi ya Rais- Fedha na Mipango*** | | | | |